# Nipashe

Jumamosi Aprili 18, 2020 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580209

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII



Th [illegible] digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710

LIKE & FOLLOW US




## Majambazi saba wauawa wakipambana na polisi

UKURASA 3


RIHANNA TAFUTA RADHI YA BABA UK.14

JUMAMOSI APRILI 18, 2020

Nipashe BT

VITA KALI

Zuchu, Ibraah Tz watoana jasho

SASA ni dhahiri kuna ushindani kati ya wasanii wa muziki wa Bongo Fleva, Harmonize na Diamond, baada ya lebo wanazoziongoza kutangaza wasanii wapya.

Wakati Msanii Diamond wiki iliyopita alimtangaza msanii mpya Zuchu, Harmonize kwa upande wake mapema wiki hii alimtambulisha Ibraah TZ, kuwa mwanamuziki ndani ya lebo ya Konde Gang. Katika kile kinachoonekana kwamba pande hizo zinafanya jambo kwa utafiti, wasanii hao wote wanaimba nyimbo zenye mahadhi ya taratibu zinazobeba hisia kali za kimahaba.

Baadhi ya watu wanadai kutambulishwa kwa wasanii hao ndio mwanzo ya vita kali ya kisanii kati ya lebo hizo mbili kwa kuwashindanisha wasanii katika soko.

UKURASA 11

# Wagonjwa asilimia 95 corona waimarika

- **Wanne** pekee wawekewa oksijeni, Polisi Dar wadaiwa kutumia bakora kutimua watu baa... *Endelea ukurasa 2,3*



### BAA LA CORONA

**SHIRIKA la Afya Duniani (WHO), limeonya Afrika huenda ikawa kitovu kipya cha mlipuko wa virusi vya corona. Onyo hilo limetokana na kuongezeka kiasi kikubwa cha visa vya ugonjwa huo wiki iliyopita.**
- **Epuka mikusanyiko ya watu**
- **Nawa mikono kwa sabuni na maji yanayotiririka**
- **Epuka kusalimiana kwa kushikana mikono na kukumbatiana**
- **Ukipiga chafya au kukohoa, ziba mdomo.**

## TANALEC kuunda mashine ya kupumulia

UKURASA 3



Muuguzi wa Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), akiwa amevaa vazi maalumu (kulia), linalokaribiana viwango na la Shirika la Afya Duniani (WHO) (kushoto), ambalo linashonwa na hospitali hiyo, kama sehemu ya mavazi ya watoa huduma (PPE), ili kujikinga wanapokuwa wanatoa huduma kwa watakaobainika kuambukizwa na virusi vya corona nchini. **Habari Uk. 3. PICHA: MNH**





Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store


## Serikali yapiga marufuku wanaokimbilia Muhimbili

UKURASA 2

**MICHEZO** **SIMBA YAIOTA UD SONGO CAF** UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6

# Kanisa Katoliki lasitisha Kwaya na mafundisho

**Na Salome Kitomari**

KANISA Katoliki nchini, limesitisha uimbaji wakati wa ibada na mafundisho ya watoto, ikiwa ni hatua ya kuepusha misongamano na kukabiliana na maambukizi ya virusi vya corona.

Kwa mujibu wa waraka uliotolewa na Katibu Mkuu wa Baraza la Maaskofu Wakatoliki Tanzania (TEC), Padri Dk. Charles Kitima, hatua hiyo ni kutekeleza agizo la Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, la kupunguza misongamano kwenye ibada.

Waraka huo wenye kumbukumbu namba TEC/MED/23/14, nakala yake imepelekwa kwa Mhadhama Polycarp Kardinali Pengo, Maaskofu Wakuu na Maaskofu.

Waraka huo ulieleza kuwa ni kwa kuzingatia maambukizi ya corona yanayoonekana pia kutoka kwenye misongamano ya watu wengi.

"Tunaomba kusitisha mazoezi ya kwaya kwa mikusanyiko na uimbaji wakati wa ibada zetu katika kipindi hiki cha mapambano dhidi ya virusi vya corona," alisema Padri Dk. Kitima.

Aidha, kanisa hilo limesitisha mafundisho ya dini kwa watoto, na kwa makundi mengine kwa njia ya mikusanyiko, na kwamba mafundisho yanaweza kufanywa kwa njia nyingine ikiwamo kuelekeza watoto wajisomee katekisimu ama kwa njia ya mtandao.

Pia, kanisa hilo limewataka waadhimishaji wa ibada kuangalia suala la muda usiwe mrefu.

"Tunawaomba waadhimishaji wa ibada na huduma mbalimbali za kikatoliki wazingatie masharti ya umbali kati ya mtu na mtu, matumizi ya vipaza sauti, kunawa mikono kabla ya kuingia kanisani, pia kunyunyuzia dawa vifaa vya ibada," alisema na kuongeza:

"Na yule anayetoa huduma ajikinge kwa umakini na kuongozwa na weledi husika kiafya kadri ya majukumu yake, mfano kuwahudumia wagonjwa na kuendesha ibada ya mazishi."

Padri Dk. Kitima alisema pia makatekista wanaokaa na wahitaji wa huduma za kiroho waeleweshwe na kupewa vifaa vya kujikinga, kufanyia usafi na unyunyiziaji dawa.



Mkuu wa Wilaya ya Kilolo, mkoani Iringa, Asia Abdallah (mwenye barakoa), akiungana na waumini wa dini ya Kiislamu wilayani humo, katika swala ya Ijumaa iliyoambatana na maombi ya nchi ya kuomba Mungu kuliepusha Taifa na janga la corona, katika uwanja wa Polisi Ilula jana. **PICHA: FRANCIS GODWIN**

# Wagonjwa asilimia 95 corona waimarika afya

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, amesema asilimia 95 ya wagonjwa wa COVID-19 waliogundulika, wanaendelea vizuri kiafya.

Kwa mujibu wa Waziri Ummy, kati ya hao wanne ndiyo wamewekewa oksijeni.

Alitoa kauli hiyo jana jijini Dar es Salaam, wakati akizindua muongozo wa huduma za afya kwa watoa huduma ngazi ya jamii.

Waziri Mwalimu alitaka wananchi kuendelea kijikinga na kijilinda dhidi ya ugonjwa huo kwa kuwa ni hatari na unaleta madhara makubwa kwa jamii.

Kuhusu muongozo uliozinduliwa, Waziri Mwalimu alisema mkakati huo wa kutumia watoa huduma za afya kwa jamii utawezesha kuwapo kwa huduma imara za kinga katika ngazi zote ikiwamo utoaji elimu ya afya na uhamasishaji kama njia muhimu ya kusaidia jamii kujikinga na magonjwa.

"Serikali inatambua kuwa jamii yenye elimu sahihi juu ya vyanzo vya afya bora na masuala yanayoweza kuathiri afya hufanya maamuzi sahihi juu ya mambo yanayohusu afya zao", alisema.

Alisema huduma hizo zitasaidia wananchi kuwa na afya njema ili kuchangia katika maendeleo yao, familia zao, jamii wanayoishi na nchi kwa ujumla.

Aliongeza kuwa, serikali imeendelea kuimarisha huduma za afya ili kufikia malengo ya upatikanaji wa huduma za afya kwa wananchi wote, ambayo itajumuisha utoaji elimu ya afya juu ya mambo yahusuyo lishe, afya ya uzazi, watoto na vijana ikijumuisha magonjwa ya mlipuko kama COVID-19 na magonjwa yasiyoambukiza.

Alisisitiza kuwa, huduma za kinga zimezingatiwa katika Sera ya Taifa ya Afya ya mwaka 2007 na Mpango Mkakati wa Sekta ya Afya wa Mwaka 2015-2020 utakuwa kipaumbele katika maandalizi ya Sera Mpya ya Afya ya Mwaka 2020.

Alisema katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita, limeshuhudia ongezeko la idadi ya watu waliopatiwa huduma za magonjwa yasiyoambukiza kutoka watu 3,386,067 mwaka 2016 hadi watu 4,190,467 mwaka 2018 ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia 24 ya wagonjwa hao.

"Pia tumeshuhudia ongezeko la vifo vitokanavyo na magonjwa yasiyoambukiza hadi kufikia asilimia 33 ya vifo vyote nchini kwa mwaka 2017, ambapo jumla ya vifo 134,600 viliripotiwa na kuhusishwa na magonjwa yasiyoambukiza," alisema.

# Serikali yapiga marufuku wanaokimbilia Muhimbili

**Na Romana Mallya**

SERIKALI imepiga marufuku Hospitali ya Taifa ya Muhimbili (MNH), kuanzia sasa kupokea wagonjwa wenye dalili za virusi vya corona, badala yake waende Hospitali ya Rufani ya mkoa, Amana.

**WAGONJWA WAFIKIA 147**

Wakati ikitoa marufuku hiyo, takwimu zilizotolewa jana na Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, zinaonyesha Tanzania ina wagonjwa wapya 53 na kufanya idadi ya wanaougua kwa sasa kufikia 147.

Waziri Ummy alisema wameamua kuanzia sasa hospitali ya Muhimbili isipokee wagonjwa hao baada ya kubaini wenye dalili za corona huenda hospitalini hapo kupata matibabu.

"Muhimbili ndiyo hospitali kuu ya Rufani ya kitaifa kwa wagonjwa wa magonjwa mengine ambayo pia inatoa matibabu ya kibingwa na bobezi ikiwamo upasuaji wa mifupa na mishipa ya fahamu na matibabu ya magonjwa ya moyo," alisema.

Alisema wananchi wote wenye dalili za corona wanatakiwa kwenda Amana kama kituo maalum cha matibabu ya ugonjwa huo.

"Wananchi wa mkoa wa Dar es Salaam wanaohitaji kupata huduma za matibabu ya magonjwa mengine katika hospitali ya Amana wanatakiwa kutumia hospitali nyingine zilizopo mkoani humo," alisema.

Kuhusu mwenendo wa ugonjwa, Waziri Ummy alisema hadi kufikia siku hiyo Tanzania ina wagonjwa wapya 53 waliokutwa na maambukizi hayo.

Alisema sampuli zilizopimwa maabara ya taifa ya Afya ya Jamii juzi zimeonyesha kuwapo kwa wagonjwa hao wapya.

"Wagonjwa wote ni Watanzania ambao wameripotiwa katika mkoa wa Dar es Salaam (38), Kilimanjaro (1), Mwanza (1), Pwani (1), Lindi (1), na Kagera (1). Wagonjwa 10 wameripotiwa kuwapo Zanzibar na kuna kifo cha mtu mmoja," alisema.

**11 WAPONA**

Alisema hadi sasa kuna jumla ya watu 147 waliopata maambukizi ya corona na kati yao waliopona ni 11 na vifo ni vitano tangu ugonjwa huu uripotiwe kuingia nchini Machi 16.

"Wagonjwa wote waliobaki 131 hali zao ni nzuri isipokuwa wanne ambao wanapatiwa matibabu ya wagonjwa mahututi kutokana na kuwa wanasumbuliwa na matatizo mengine ya kiafya," alisema.

**HALI ZANZIBAR**

Kwa upande wa Waziri wa Afya, Zanzibar, Hamad Rashid Mohammed, alisema visiwani humo kuna jumla ya wagonjwa 11 wenye umri kati ya miaka 22 mpaka 66 na kufanya jumla ya watu wanaougua kufikia 35.

Aidha, alisema kati ya watu hao wanawake ni wanne na wanaume saba ambao wote wanaendelea na matibabu.

Kwa mujibu wa takwimu za Shirika la Afya Ulimwenguni (WHO), hadi jana duniani kuna visa 2,074,529 walioambukizwa corona, kati yake watu 139,378 wamepoteza maisha, huku visa 1,050,871 vikiwa bara la Ulaya, 743,607 viko Marekani, 127,595 viko Pasifiki Magharibi, 115,824 viko Mashariki ya Meditereniani, 23,560 viko kusini mwa Asia na 12,360 barani Afrika.

## Tanalec kutengeneza mashine ya kupumulia

**Na Waandishi Wetu**

KIWANDA cha Tanelec cha jijini Arusha, kimeanza kufanya utafiti wa mashine za kusaidia wagonjwa kupumulia katika kudhibiti virusi vya corona na magonjwa mengine.

Meneja Msaidizi wa Tanalec, Michael Mangowi, alisema hayo kwenye hafla fupi ya makabidhiano kwa serikali mkoa wa Arusha ya vifaa vya kutakasa mikono vikiwamo sabuni 100 na ndoo 100, kwa ajili ya kujikinga na ugonjwa wa corona.

Alisema taasisi hiyo kupitia wafanyakazi wake imeendelea na utafiti wa kutengeneza mashine hizo pamoja na nyingine ya kupita na kumwagia dawa ya kutakasa mwili mzima kwa lengo la kuendelea na mapambano dhidi ya ugonjwa huo.

"Tumejipanga kuhakikisha tunaendelea na utafiti wa kuhakikisha tunapambana na ugonjwa huu kusaidia vitakasa mikono na mwili, ili kuisaidia serikali yetu dhidi ya janga la ugonjwa huu,"alisema.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Mrisho Gambo, aliIshukuru kwa msaada huo, kwa kuwa ugonjwa huo hauchagui viongozi wala mtu.

Alisisistiza kuwa mkoa huo umejidhatiti kuimarisha udhibiti wa wahamiaji haramu wanaoingia maeneo ya mipaka hasa wa Namanga, wilayani Longido, pamoja na mpaka wa Ngorongoro uliopo wilayani Ngorongoro unaopakana na nchi jirani ya Kenya.

Mmoja kati ya wanufaika wa msaada huo, Mwenyekiti wa stendi kuu ya mabasi, Maulid Rajabu, alishukuru kwa na kuahidi kuendelea kutoa elimu ya ugonjwa huo na kuhakikisha kila basi linakuwa na ndoo pamoja na sabuni kwa ajili ya kunawia mikono.

**MNH YASHONA VAZI KUJIKINGA CORONA**

Nayo Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), imeshona vazi maalumu ambalo ni sehemu ya mavazi ya watoa huduma (PPE) katika hospitali hiyo kwa watu watakaobainika kuambukizwa ugonjwa wa Covid-19 unaosababishwa na virusi vya corona.

Akizungumza, Mkurugenzi wa Huduma za Tiba wa Muhimbili, Dk. Hedwiga Swai, alisema jitihada hizo ni katika kuunga mkono juhudi za serikali katika ugonjwa huo unaolikumba taifa na dunia kwa ujumla.

"Kwa sasa hivi upatikanaji wa hili vazi kote duniani ni adimu na kama serikali ni lazima tuwalinde wafanyakazi wetu wa afya," alisema Dk. Swai.

Alisema PPE zinazotoka nje ya nchi hugharimu fedha nyingi za Tanzania na kwa vazi moja ni kati ya Sh. 350,000 hadi Sh. 500,000 kutegemea na nchi liliponunuliwa na linaloshonwa Muhimbili hugharimu Sh. 30,000 gharama ambayo watoa huduma huimudu.

■**Imeandikwa na Enock Charles (Dar) na Cynthia Mwilolezi, Arusha**

# Majambazi 7 wauawa wakipambana na polisi

**Na Pendo Thomas,** KIGOMA

WATU saba wanaosadikiwa kuwa majambazi wameuawa baada ya majibishano ya kurushiana risasi na polisi wakati wakienda kutekeleza uhalifu katika kampuni ya ujenzi wa barabara ya Sino hydro engineering construction ya mjini hapa.

Akithibitisha kutokea kwa tukio hilo jana, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kigoma, ACP Martin Otieno, alisema tukio hilo limetokea juzi saa tano usiku baada ya jeshi hilo kupokea taarifa ya kikundi kinachopanga kwenda kutekeleza uhalifu huo.

Kamanda Otieno alisema kufuatia taarifa hizo, kikosi kazi kilijipanga kwenda kuimarisha ulinzi katika maeneo ambayo walipanga kujificha na baadaye kuona kundi la watu 12 wakitembea kuelekea kutimiza azma yao na walipobaini kuwa wanafuatiliwa walianza kuwarushia risasi askari na kuibuka majibizano ya risasi yaliyodumu kwa takribani dakika 25.

Pia, Kamanda Otieno alisema katika majibizano hayo askari waliwaua majambazi watatu hapo hapo na wanne walikufa njiani wakati wakipelekwa hospitali ya wilaya ya Kibondo huku wengine watano wakikimbia kusikojulikana.

Jeshi hilo pia limekamata bunduki tatu zilizotengenezwa kienyeji, pisto moja, risasi 89 za SMG, 15 za pisto na kofia za kuficha sura ambazo zilikuwa zikitumika katika uhalifu.

Vilevile Otieno alitoa onyo kali kwa wananchi wanaojiingizia kipato kupitia shughuli za uhalifu na kuwa wanaendelea na msako wa kuwabaini na hatua kali dhidi ya watakaobainika zitachukuliwa ili kuwezesha wananchi wa mkoa huo kuishi salama bila hofu.

"Napenda kutoa wito kwa wote wanaofanya shughuli haramu katika mkoa wa Kigoma na kusumbua wananchi na wawekezaji, kitu hiki hakikubaliki na tutaendelea kuwashughulikia kama hawa saba," alionya.

Katika siku za hivi karibuni kumekuwapo na matukio ya ujambazi yanayohusishwa na raia kutoka nchi jirani ya Burundi, jeshi hilo limesema hadi sasa halijatambua wahusika wa tukio hilo kama ni kutoka nchi jirani au ni Watanzania.



Mkuu wa Wilaya ya Bariadi, mkoani Simiyu, Festo Kiswaga (wa pili kushoto), akikagua mnada wa mazao wa Dutwa juzi, ili kujua bei ya vyakula mbalimbali hasa wakati huu wa mlipuko wa maambukizi ya virusi vya corona. **PICHA: HAPPY SEVERINE**

# Polisi Dar wadaiwa kuwatimua watu baa

**Na Romana Mallya**

KATIKA kudhibiti kusambaa kwa virusi vya corona, askari polisi wamedaiwa kutumia viboko kuwatawanya watu waliokuwa baa mbalimbali jijini Dar es Salaam.

Aidha, wanadaiwa kutumia king'ora cha polisi kuwataka watu kuondoka katika baa kwenye maeneo kadhaa juzi.

Nipashe ilishuhudia juzi usiku maeneo mbalimbali watu waliokuwa baa wakiendelea na upataji wa vinywaji wakipigwa viboko kama namna ya kuwatawanya.

Serikali mara kwa mara tangu mlipuko wa corona uingie nchini, imekuwa ikiwataka wananchi kuchukua tahadhari ikiwamo kuepuka mikusanyiko isiyo ya lazima.

Juzi, askari wakiwa na magari, walipita baa mbalimbali na kuwataka watu waliokuwamo watawanyike, na waliokaidi walitawanywa kwa nguvu ikiwamo kutumia bakora.

Gazeti hili lilishuhudia eneo la Sinza Mori namna wateja walivyokuwa wakikimbia na kuacha vinjwaji vyao mezani na magari yao.

Maeneo mengine ambayo watu walijikuta wakichapwa ni waliokuwa kwenye mikusanyiko ikiwamo baa na grosari katika mitaa ya Kinondoni.

**KAMANDA MAMBOSASA**

Kamanda wa Polisi wa Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Lazaro Mambosasa, alipoulizwa kuhusiana na suala hilo, alisema maelezo waliyotoa kwa askari, ni kuwa wapite maeneo yenye mikusanyiko ikiwamo baa ili kuwapa elimu ya athari za mikusanyiko nyakati hizi.

"Hatujawatuma askari kwenda kuwachapa waliokaa baa, tumewatuma kwa kuwapa elimu na elimu hii itolewe maeneo yote yenye mikusanyiko.

"Kama wamewachapa watu hicho ni kinyume cha sheria, Jeshi la Polisi hatujafundishwa kuchapa mtu viboko, kama mtu amekaidi wanapaswa kumkamata na kumpeleka kituoni kwa hatua nyingine."

Kamanda Mambosasa alisema kumpiga mtu kiboko ni kosa la jinai kwa sababu hakuna sheria inayowaelekeza hivyo."Kupiga kiboko ni adhabu ambayo hutolewa na mahakama na wapo maofisa Magereza ambao wamesomea hiyo kazi," alisisitiza.

Kutokana na hali hiyo kujitokeza juzi, Kamanda Mambosasa aliwataka askari wanaokwenda mtaani wakatoe elimu kuhusu athari za mikusanyiko dhidi ya corona, na kwamba wakaidi wakamatwe.

**RPC KINONDONI**

Naye, Kamanda wa Polisi wa mkoa wa Kipolisi Kinondoni, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi, Edward Bukombe, alithibitisha kuwa juzi walianza msako wa kuwaondoa watu kwenye mikusanyiko ikiwamo baa, lakini hana taarifa kama kuna watu walichapwa kwenye operesheni hiyo.

"Tumeanza operesheni hii jana (juzi) na itakuwa endelevu, baa ambazo zinakiuka mamlaka za serikali zilizotaka watu wasikusanyike tutapita kote... unakuta watu wamejikusanya kana kwamba hawajui nini kinachoendelea duniani," alisema Bukombe.

"Wamejikusanya bila kuchukua tahadhari yoyote, msako ndo umeanza na watakaokaidi tutawakamata."

**DC ILALA ANENA**

Mkuu wa Wilaya ya Ilala, Sophia Mjema, amewataka wamiliki wa baa wilayani humo kuanzia jana hawaruhusiwi kuwapo kwa mikusanyiko ya watu kwenye baa.

Mjema alisema vinywaji vitauzwa na mnunuzi atapaswa kunywea nyumbani na siyo baa, na ambaye hatazingatia maelekezo hayo, hatua za kisheria zitachukuliwa kwa mmiliki, mwendeshaji na mtu yeyote atakayeonekana maeneo hayo akinywa.


**UTHIBITISHO WA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**Katika Mahakama ya Mwanzo MWANGA MJINI**
**Mirathi Na. 07/2020**
**Maombi ya barua za usimamizi wa Mirathi ya Marehemu HADIJA HAMISI MRUTU**
**na**
**RASHIDA ALI AMIRI.........WAOMBAJI**

**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(Kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki ya marehemu iliyotajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua za usimamizi wa Mirathi kwa waombaji hapo juu. Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 27 mwezi 04..2020.

Imewasilishwa MWANGA leo tarehe 3 mwezi 03..2020.

HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA MWANZO
MWANGA

1157065

# Ulanguzi biashara sukari wafichuka

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

SIKU moja baada ya serikali kuonya kuhusu kupaa kwa bei ya sukari nchini, imebainika kupanda kwa bei ya bidhaa hiyo kumetokana na baadhi ya wafanyabiashara kufanya ulanguzi kwa lengo la kupata faida kubwa.

Jana, Nipashe iliripoti kuhusu kupaa kwa bei ya sukari kwenye maeneo mbalimbali nchini ikiuzwa kati ya Sh. 2,800 na 4,500 kwa kilo, isipokuwa visiwani Zanzibar ambako iliuzwa kwa bei ya Sh. 1,800 kwa kilo.

Kutokana na hali hiyo, serikali kupitia kwa Waziri wa Viwanda na Biashara, Innocent Bashungwa, ilisema itachukua hatua kali za kisheria dhidi ya wafanyabiashara watakaobainika kuficha sukari kwa lengo la kupandisha bei wakati huu wa janga la corona.

Waziri Bashungwa pia alisema serikali imeunda timu ya kufuatilia suala hilo na imeagiza zaidi ya tani 20,000 za sukari nje ya nchi ikiwa ni tahadhari ya kuwa na akiba ya kutosha ya bidhaa hiyo katika kipindi hiki cha baa la corona.

Wakati serikali ikichukua hatua hizo, uchunguzi uliofanywa na Nipashe ukihusisha mahojiano na baadhi ya wafanyabiashara wa sukari nchini, umebaini kupaa kwa bei hiyo kumetokana na tamaa ya baadhi ya wafanyabiashara kupata fedha nyingi kupitia ulanguzi katika bei ya bidhaa hiyo.

Gazeti hili limebaini kuwa gharama za kuagiza bidhaa hiyo nje ya nchi zinafikia Dola 757.47 (Sh. 1,748,080) kwa tani moja. Mchanganuo wake ni: Cost+insurance+freight Dola 425 (Sh. 980,810) kwa tani, duty (35%) Dola 148.75 (Sh. 343,283) kwa tani, VAT (18%) Dola 104.82 (Sh. 241,902), clearing and transport Dola 70.29 (Sh.162,214) kwa tani.

"Kwa mantiki hiyo, mfuko wa Kg 50 wa sukari unagharimu Dola 37.8 (Sh. 87,677) na ukijumulisha na faida ya asilimia nane (7,400), unaona kwamba mfuko huo unapaswa kuuzwa kwa Sh. 95,000 (Sh. 1,900 kwa kilo) na si 130,000 inayofanyika sasa," alisema mmoja wa wafanyabiashara hao ambaye aliomba hifadhi ya jina lake.

**UPINZANI WAJA JUU**

Akizungumza na Nipashe bungeni jijini hapa jana, Waziri Kivuli wa Viwanda na Biashara, David Silinde, alisema Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka serikali kutoa taarifa bungeni kuhusu hali halisi ya upatikanaji wa sukari nchini.

Silinde ambaye pia ni Mbunge wa Momba (Chadema), alisema serikali pia inatakiwa kuliambia Bunge mikakati inayochukuliwa kuhakikisha nchi inakuwa na uhakika wa upatikanaji wa bidhaa hiyo.

"Sukari kupanda bei ni matokeo ya serikali kushindwa kuchukua hatua kabla. Sukari imepanda bei kwa sababu viwanda vya ndani vimeshindwa kuzalisha kwa kiwango kinachotakiwa na mvua sasa inanyesha sana. Ni uzembe mdogo kwa sababu jambo hili lilipaswa kutatuliwa kabla.

"Serikali ilipaswa kuagiza sukari mapema. Tumezuia uagizaji wa sukari ili viwanda vya ndani vizalishe, lakini kwenye sheria ya sukari tuna kipengele kinatupa nafasi ya kuagiza. Jana na juzi kuna kiwanda kimeagiza tani 9,000, lakini hizi sisi tunaona hazitoshi.

Nipashe pia iliitafuta Bodi ya Sukari kuzungumzia suala hilo jana, lakini maofisa wa idara yake ya mawasiliano walidai Mkurugenzi Mkuu yuko safarini na atalizungumzia baada ya kurejea ofisini.

## Kizimbani tuhuma uhujumu uchumi

**Na Hellen Mwango**

MFANYABIASHARA Msiniege Mwakatumbula (56), mkazi wa Bunju, jijini Dar es Salaam, amefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, akikabiliwa kesi ya uhujumu uchumi.

Anakabiliwa na makosa ya kukutwa na madini na kutakatisha Dola za Marekani 2,950.73 (sawa na Sh.6,791,518.20).

Mshtakiwa huyo alisomewa mashtaka yake mbele ya Hakimu Mkazi, Vick Mwaikambo.

Wakili wa Serikali Mwandamizi, Wankyo Simon, alidai Machi Mosi, mwaka huu eneo la Bunju 'B', jijini Dar es Salaam, mshtakiwa alikutwa akifanya biashara ya madini isivyo halali.

Ilidaiwa mshtakiwa alikutwa isivyo halali akifanya biashara ya madini ya rubbi, corundum, hessonite na sapphirenuts.

Mengine ni moonstones, garnet na beryl yenye uzito wa gramu 6451.80 yakiwa na thamani ya kiasi hicho cha fedha. Ilidaiwa madini hayo ni mali ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania.

Shitaka la pili, siku, tarehe na mahali pa tukio la kwanza, mshtakiwa alitakatisha fedha hizo huku akijua madini hayo ni mali ya serikali.

Mshtakiwa hakutakiwa kujibu chochote kwa kuwa mahakama hiyo haina mamlaka ya kusikiliza kesi za Uhujumu Uchumi.

Hakimu Mwaikambo alisema kesi hiyo itatajwa Mei 4, mwaka huu na mshtakiwa apelekwe mahabusu.




Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Zainab Telack (kushoto), akipokea vifaa vya kujikinga na maambukizi ya virusi vya corona, kutoka kwa Mkuu wa Kitengo cha Afya na Usalama Kazini wa kampuni ya uchimbaji wa madini ya dhahabu ya Barrick Buzwagi, wilayani Kahama, jana.
**PICHA: MARCO MADUHU**

# Mahakama ya Mafisadi yaokoa mabilioni kesi 49 zikinguruma

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

KUANZISHWA kwa Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi, maarufu Mahakama ya Mafisadi, ndani ya Mahakamu Kuu, kumeisaidia serikali kuokoa mabilioni ya shilingi, imeelezwa.

Hayo yalibainisha na Waziri wa Katiba na Sheria, Balozi Dk. Augustine Mahiga, alipowasilisha bungeni jijini hapa jana, makadirio ya mapato na matumizi ya wizara yake kwa mwaka ujao wa fedha.

Dk. Mahiga alibainisha kwamba, katika kipindi cha kuanzia Julai 2019 hadi Machi 2020, Divisheni hiyo ilisajili jumla ya kesi 49 za rushwa na uhujumu uchumi na kesi 40 zimetolewa uamuzi.

Alisema thamani ya mali zilizorejeshwa au kutaifishwa kutokana na kesi hizo ni jumla Sh. bilioni 29.9 zikiwamo magari mawili, nyumba moja, ghorofa moja na fidia ya Sh. bilioni 26.3.

"Katika kipindi cha Julai 2019 hadi Machi 2020, Wizara kupitia Ofisi ya Taifa ya Mashtaka imeendesha jumla ya kesi kubwa tano (5) katika Mahakama Kuu Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi ambapo washtakiwa waliotiwa hatiani kutokana na kesi hizo walipewa adhabu mbalimbali zikiwamo vifungo, faini, fidia kwa Serikali na mali mbalimbali kutaifishwa.

"Kiasi cha Sh. 32,534,528,871.20 (Sh. bilioni 32.534) kilipatikana kama fidia kwa serikali, Sh. 205,500,000 (milioni 205.5) kilipatikana kama faini na nyumba mbili zilitaifishwa kuwa mali ya serikali kwa amri ya mahakama.

"Aidha, baada ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 11 ya Mwaka 2019, katika zoezi la washitakiwa kukiri makosa yao (plea bargain), jumla ya Sh. 15,638,464,678.17 (Bilioni 15.638) zimeshalipwa kama kodi iliyokwepwa, faini na fidia baada ya washitakiwa 381 kukiri makosa yao na kulipa fedha katika akaunti maalum iliyopo Benki Kuu ya Tanzania na zoezi la urejeshaji wa fedha kwa wale ambao hawajamaliza linaendelea," alibainisha.

Dk. Mahiga pia alisema wizara kupitia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, imeendelea kufanya majadiliano na upekuzi wa mikataba mbalimbali ya kitaifa, kikanda na kimataifa.

Alisema kuwa katika kipindi cha kuanzia Julai 2019 hadi Machi 2020, jumla ya mikataba ya kitaifa na kimataifa 770, sawa na asilimia 57, ilifanyiwa upekuzi kati ya Mikataba 1,333 iliyokuwa imepangwa.

"Kati ya mikataba 770 iliyofanyiwa upekuzi, 345 ilikuwa imethaminishwa katika sarafu mbalimbali. Mikataba 262 ilikuwa na thamani ya Sh. 4,645,372,100,000, mikataba 61 ilikuwa na thamani ya Dola za Marekani 6,011,297,150.38, sawa na Sh. 14,036,979,975,852.30, mikataba 22 ilikuwa na thamani ya Euro 118,566,870.31 (Sh. 299,508,463,074.41).

"Mikataba hiyo ilihusisha masuala ya ununuzi, ujenzi na ukarabati wa majengo, utoaji wa huduma za jamii kama vile ujenzi wa shule, hospitali na barabara.

## Corona yakwamisha kesi ya 'Mpemba'

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, imeshindwa kuendelea kusikiliza ushahidi wa Jamhuri wa kesi ya uhujumu uchumi inayomkabili Yusuf Ali maarufu kama 'Mpemba wa Magufuli', kwa sababu ya kujikinga na maambukizi ya virusi vya corona.

Hatua hiyo imefikiwa baada ya upande wa Jamhuri kushindwa kuwaita mashahidi katika kipindi hiki mpaka pale hali itakapoimarika.

Kesi hiyo ilitajwa katika Mahakama Mtandao iliyoketi chini ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Rashid Chaungu, baada ya Hakimu Mkazi Mkuu, Thomas Simba, kuwa na udhuru.

Wakili wa Serikali Mwandamizi, Wankyo Simon, alidai kesi ilipangwa kwa ajili ya kuendelea kusikilizwa, lakini kutokana na tishio la maambukizi ya virusi vya corona, wameshindwa kuita mashahidi.

Kutokana na hali hiyo, alisema Jamhuri inaomba tarehe nyingine ya kutajwa, ambapo Hakimu Chaungu alisema itatajwa Aprili 30,mwaka huu na kwamba washtakiwa wataendelea kukaa mahabusu.

Kabla ya kuahirishwa kesi hiyo mshtakiwa wa pili, Ernest Mrutu, aliomba mbele ya mahakama hiyo kuwa Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) amwachilie kwa madai kuwa ndugu zake wamemuarifu kuwa wameshalipa Sh.milioni 15 ambazo ni sehemu ya makubaliano baada ya majadiliano ya kukiri na kuomba msamaha.

Akijibu hoja hiyo, Wakili Wankyo alidai hana taarifa kuhusu jambo hilo, na kuwa majadiliano kati ya ndugu wa mshtakiwa na DPP yanaendelea, hivyo yatakapokamilika, ataiarifu mahakama hiyo.

Yusuph na wenzake watano wanakabiliwa na mashtaka manne, ikiwamo kujihusisha na biashara haramu ya meno ya tembo yenye thamani ya Sh. milioni 785.



Mafundi wakiandaa msingi kwa ajili ya ujenzi wa Seko Sekondari, iliyopo Kata ya Nyamrandirira Musoma Vijijini mkoani Mara juzi, ambayo inajengwa na serikali huku wananchi wakichangia fedha na nguvu kazi. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# Wananchi waitikia wito wa JPM kufanya maombi

**Na Romana Mallya**

MAKUNDI mbalimbali ya jamii, yameitikia wito wa Rais John Magufuli, alioutoa kwa Watanzania wa kumuomba Mungu kwa siku tatu mfululizo dhidi ya virusi vya corona.

Juzi, Rais Magufuli kupitia ukurasa wake wa Twitter, aliandika ujumbe mfupi usemao, "Ndugu zangu Watanzania, kutokana na ugonjwa wa corona.

"Nawaomba tutumie siku tatu za kuanzia Aprili 17 (Ijumaa, Jumamosi na Jumapili) kumuomba Mwenyezi Mungu aliye muweza wa yote atuepushe na janga la ugonjwa huu. Tusali kwa kila mmoja kwa imani yake, atatusikia."

Baada ya ujumbe huo kusambaa mitandao mbalimbali ya kijamii, watu wakiwamo viongozi wa siasa, waliandika kwenye ukurasa wa Rais kumuunga mkono.

Mbunge wa Arusha Mjini, Godbless Lema, katika ukurasa huo wa Rais aliandika, "Rais, Mimi na familia yangu tutafunga na kuomba kwa hizo siku tatu. Ubarikiwe."

Kiongozi Mkuu wa ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe aliandika, "Ndugu zangu Watanzania, kutokana na ugonjwa wa corona, nawaomba tuendelee kuepuka mikusanyiko.

"Kunawa mikono yetu kwa maji na sabuni mara kwa mara na kuzingatia maelekezo ya Wataalamu wa Afya. Mungu atatusikia iwapo tutajitahidi kujikinga na maambukizi."

Mmoja wa watumiaji wa Twitter aliandika kwenye ukurasa huo wa Rais Magufuli, "Amen Rais wetu tunajivunia sana kuwa na mzee mwenye kuguswa na mwenye upendo wa dhati kwa watu unaowatumikia.

"Tutamuomba Mungu na naimani atatusikia kwani Mungu wetu ni Mungu mwenye upendo pia. Amina."

Naye, De_eyez aliandika, "Ikiwa watu wangu, walioitwa kwa jina langu, watajinyenyekesha na kuomba na kunitafuta uso na kuziacha njia zao mbaya basi nitasikia toka mbinuni na kuwasamehe dhambi yao na kuiponya nchi yao."

"Mheshimiwa Rais leo nimeona Tweet yako kuna kitu kwenye nafsi yangu kimeniambia hakika wewe ni mtu ambaye una imani kubwa sana ya Mungu," aliandika Rahma Hassani na kuongeza:

"Na ukweli ni huo kila kauli yako umekuwa ukitusisitiza tuombe kila mtu kwa imani yake, hakika na sisi tunaomba, tutaomba na tutaendelea kuomba."

Naye, Robby Chriss aliandika, "Ni jambo la muhimu sana kumuomba Mungu...hii inaonesha imani kubwa kwa aliyetuumba...lakini pia tuzidi kujikinga na kufuata hatua zingine za kujihami tukiendelea kusubiri maombi yetu yatimie. Mungu ibariki Tanzania."

Kwa upande wake, Robert Mhando aliandika, "Rais hakika unatuongoza katika njia sahihi, tumepokea agizo lako tutafunga na kuomba Mungu atuongoze Watanzania tuendelee kuchukua tahadhari dhidi ya maambukizi ya virusi vya corona."

Katika kurasa mbalimbali za Facebook, Instagram na WhatsApp, watu mbalimbali wametuma mistari mbalimbali ya vitabu vya Mungu kama mwongozo wa safari hiyo ya siku tatu ya maombi.

Wengine wamekumbushana pamoja na maombi, pia, yaambatane na kufunga kwa siku hizo tatu.

Chombo kimoja cha habari kimewataka wananchi popote walipo wakifanya ibada na maombi katika kuliomba taifa dhidi ya corona, wayatume kwa njia ya video fupi isiyozidi dakika moja kupitia ukurasa wao wa 'WhatsApp'.

Katika eneo la Mnazi mmoja, wananchi walionekana wakiwa wanasali kwa kuachiana umbali uliopendekezwa kitaalamu.

**KILOLO NAO WAFANYA MAOMBI**

Mkuu wa Wilaya ya Kilolo, mkoani Iringa, Asia Abdallah, na kamati yake ya ulinzi na usalama aliungana na waumini wa dini ya Kiislamu katika wilaya hiyo kufanya maombi ya kuliombea taifa, iliyofanyika katika viwanja vya polisi mjini Ilula.

Akitoa salamu kwa waumini hao baada ya ibada, Mkuu huyo wa wilaya alisema kuwa huu si wakati wa kuchukulia poa, na kwamba hatua zilizochukuliwa na wilaya hiyo ni kuagiza watendaji wa vijiji na kata zote kufanya msako mitaani na kuwachukulia hatua kali wote watakaobainika wakikiuka kanuni za afya.

Mkuu huyo wa wilaya alisema, pamoja na kuomba Mungu bado wananchi wote wanakumbushwa kuacha kutenda matendo ambayo ni kikwazo mbele za Mungu, japo wale ambao wataweza kufunga na kuomba basi wafanye hivyo wakati huo wa siku tatu za kumuomba Mungu.

■**Imeandikwa na Romana Mallya (DAR) na Fransis Godwin (IRINGA)**

# Mahakamani lazima barakoa

**Na Enock Charles**

UONGOZI wa Mahakama nchini, umewataka wadau wa mahakama kuvaa barakoa (mask) wakati wa kwenda kupata huduma katika mahakama ili kujikinga na maambukizi ya virusi vya corona.

Katika taarifa iliyotolewa jana kwa vyombo vya habari na Mtendaji Mkuu wa Mahakama, wananchi wametakiwa pia kuhakikisha wananawa mikono kwa maji tiririka na vitakasa mikono wanapoingia na kutoka mahakamani.

"Uongozi wa Mahakama ya Tanzania, unawatangazia wadau wote wa Mahakama pamoja na wananchi kwa ujumla kuwa, kuanzia siku ya Jumatatu, Aprili 20, mwaka huu, wadau wote wakiwemo wananchi wanaofika mahakamani kupata huduma watatakiwa kuvaa barakoa."

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Klabu, wachezaji Tanzania watakiwa kujiweka tayari

**WAKATI** bado hatima ya Ligi Kuu Bara msimu huu wa mwaka 2019/20 haijajulikana kutokana na kuwapo kwa sakata la ugonjwa wa corona (COVID 19), klabu za Tanzania zinatakiwa kuanza maandalizi ya msimu mpya mapema.

Ligi Kuu Tanzania Bara ilisimama wakati zikiwa zimesalia mechi 10 ili msimu umalizike, wakati Ligi Daraja la Kwanza zilikuwa imebakia michezo michache.

Nipashe inazitaka klabu za Simba, Yanga, Azam FC na klabu nyingine kuanza mapema maandalizi ya msimu ujao wa Ligi Kuu Bara na mashindano ya kimataifa, kwa sababu lolote linaweza kutokea.

Hadi kufikia jana mchana, Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), lilikuwa bado halijatoa mwongozo mpya wa kuhusiana na msimu huu utamalizikaje, lakini ni vema timu zote zikaanza kujipanga mapema.

Usajili wa wachezaji wapya au kuwaongezea nyota mikataba mipya na kuanza mapema maandalizi kwa ajili ya kumalizia msimu na kuanza msimu mpya kutasaidia kuziweka timu zote tayari na mapambano mara uamuzi mpya utakapotolewa.

Hii itazifanya klabu zote kuwa imara na kumalizia msimu kwa ushindani na hatimaye wawakilishi watakaopatikana wawe na uwezo wa kupambana na si kwenda kusindikiza klabu za mataifa mengine.

Kimsingi msimu bado haijamalizika, hivyo viongozi, wachezaji na maofisa wote wa timu zetu wanatakiwa kutolala na badala yake kuimarisha idara zote za timu kwa malengo ya kumaliza msimu kishujaa.

Tunafahamu soka ni mchezo usiotabirika, Simba, Yanga, Azam na klabu nyingine, hampaswi kukata tamaa kuelekea na matokeo yake kujiandaa kuendelea na mapambano na mara uamuzi wa kushiriki mashindano ya kimataifa ukitolea, nchi inakuwa na wawakilishi imara.

Kimahesabu ni kama Simba inaonekana kuwa na nafasi nzuri ya kushiriki mashindano ya kimataifa ya msimu ujao kwa sababu ni mabingwa watetezi na vile vile ni vinara katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara ambayo inashirikisha klabu 20.

Kikubwa kuelekea kwenye hatua ya lala salama au msimu mpya, makocha wanapaswa kujipanga imara kukabiliana na ushindani kwa sababu mechi za hatua ya lala salama huwa hazitabiriki wakati zile za michuano ya kimataifa huwa ngumu zaidi.

Katika dunia ya sasa hakuna timu ndogo, hakuna mchezaji mkubwa, timu inayojiandaa vema ndiyo timu inayojiweka katika mazingira bora ya kushinda mataji.

Simba, Yanga na Azam FC ambao ni mabingwa watetezi wa mashindano ya Kombe la FA, mnatakiwa kuwa mfano kwa timu nyingine kuhakikisha mnafuatilia kwa makini maendeleo ya wachezaji wenu katika kipindi hiki, na mara hali ya kawaida itakaporejea, wadau waendelee kushuhudia soka la kuvutia.

Hakuna kitu kisichowezekana, kama wachezaji watafuata misingi ya kujituma na kufanya mazoezi kulingana na maelekezo waliyopewa, watalinda viwango vyao na hatimaye kupata matokeo mazuri, pale mechi za ushindani zitakaporejea.

Nipashe tunaamini timu zetu zinaweza zikafanya vizuri na kuipeperusha vema bendera ya Tanzania katika ligi za ndani na mashindano ya kimataifa kama wachezaji watalinda viwango vyao katika muda huu ambao ligi na michuano mbalimbali imesimama.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Kinywa jumba la maneno

Na Barnabas Maro

**KINYWA** cha binadamu ni kama jumba la maneno. Methali hii hutumiwa kutukumbusha kuwa binadamu ana uwezo wa kusema maneno yoyote, yawe mazuri au mabaya. Hatupaswi kushangaa tusikiapo mtu kasema maneno fulani.

Vile vile husemwa "Ulimi huuma kuliko meno." Tunakumbushwa kuwa maneno anayotamka mtu yana uwezo wa kuleta maumivu au kumuumiza mtu sana. Tunashauriwa tuyapime maneno kabla ya kuyasema ili yasije yakawaudhi na kuwakera wenzetu.

Aidha, "maneno ni kama fumo, yakitoka mdomoni hayarudi." Maana yake neno analotamka mtu ni kama mkuki, likitoka halirudi na huweza kuleta madhara.

Methali hii yatunasihi tuwe na tabia ya kuyatafakari maneno tusemayo. Ni vizuri kulipima neno kabla ya kulisema na kujiletea majuto baadaye.

'Siri' ni jambo lililo moyoni mwa mtu asilolijua mwingine ila yeye tu. Habari au jambo ambalo watu wengi hawalijui; jambo lililofichika au tukio ambalo bado halijatakiwa kuwekwa bayana au kudhihirishwa.

Huwa najiuliza lakini sipati jibu. Viongozi wanaotoa siri za vilabu vyao vya kandanda huwashwa midomo, hupewa rushwa ili watoe siri za vilabu vyao, au ni silika (tabia alizonazo mtu tangu alipozaliwa na kukua nazo)?

Tunaambiwa Yanga na Simba ni watani wa jadi. Viongozi, wanachama na mashabiki wa timu hizo wanaelewa maana ya utani? Maana ya 'utani' ni maneno au vitendo vya dhihaka; tabia ya watu kufanyiana masihara kwa lengo la kuambiana kweli na kuimarisha uhusiano wao.

Kwa utaratibu huo, 'watani' ni watu aghalabu wa makabila tofauti au marafiki wakubwa wanaoruhusiwa kudhihakiana kwa mujibu wa mila zao bila wanaotaniwa kukasirika.

Sioni 'utani' wa Yanga na Simba ingawa mwanzoni (mwaka 1935) walikuwa timu moja na baadaye kundi moja likajitoa na kuunda timu iliyoitwa Sunderland, mji ulio pwani ya Kaskazini Mashariki ya Uingereza.

Huo ni utani au utengano (hali au tendo la kuachana au kukaa mbalimbali na mtu/ watu wengine bila kushirikiana)?

Nchini Tanzania kabila lenye watani wengi zaidi ni Wangoni ambao chimbuko (asili) lao ni Afrika Kusini.

Kabila hili limeenea katika nchi mbalimbali za Afrika wala isidhaniwe ni Tanzania tu.

Je, Yanga na Simba ni 'watani wa jadi' kama isemwavyo? 'Jadi' ni mambo ya asili ambayo watu wa kabila fulani hurithi kutoka kwa mababu zao; asili ya mtu kama vile uzawa, ukoo au nasaba.

Timu hizo zimerithi chuki (hisia ya kutopenda kitu au jambo) na visasi (matendo wanayofanya watu kwa wengine kulipiza mabaya waliyofanyiwa; dhamiri za kuwafanyia wengine ubaya kulipiza visasi walivyofanyiana) kutoka kwa mababu zao? N'nani aliyewadanganya kuwa mababu zao walikuwa na tabia hiyo mbaya?

Kwa Yanga na Simba mambo hayo hayamo kabisa kwenye fikra (mawazo yaliyomo vichwani mwa timu hizo) zao! 'Chukia' ni kitendo cha mtu kutopenda mtu mwingine au kitu. 'Chukiza' ni kitendo cha kufanya jambo la kuudhi. Kitendo cha kiumbe kufika kiwango cha kutopendeza kwa wengine kutokana na matendo yake.

Mambo yafanywayo na Yanga na Simba si 'utani wa jadi' kama isemwavyo, bali ni chuki za wazi zisizokuwa na kificho. Timu hizo huombeana mabaya na hata kuendeana kwa wachawi usiku wa kiza totoro na mchana wa jua la utosini ili upande mwingine udhurike!

"Amelaaniwa mtu yule amtegemeaye mwanadamu, amfanyaye mwanadamu kuwa kinga yake, na moyoni mwake amemwacha Bwana.

Maana atakuwa kama fukara nyikani, hataona yatakapotokea mema. Bali atakaa jangwani palipo ukame, katika nchi ya chumvi isiyokaliwa na watu.

"Amebarikiwa mtu yule anayemtegemea Bwana, ambaye Bwana ni tumaini lake. Maana atakuwa kama mti uliopandwa kando ya maji uenezao mizizi yake karibu na mto; hautaona hofu wakati wa hari ujapo, bali jani lake litakuwa bichi; wala hautahangaika mwaka wa uchache wa mvua, wala hautaacha kuzaa matunda." (Yeremia 17:5-8).

Sasa Simba imeishitaki Yanga kwa kutaka kumsajili mchezaji wao, Clatous Chama ilhali kulikuwa na tetesi kuwa Simba ilitaka kumsajili Papy Tshishimbi ingawa imekanushwa vilivyo na msemaji wa Simba, Haji Manara. Suala hilo sasa linashughulikiwa na Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), baada ya Makamu Mwenyekiti wa Yanga, Frederick Mwakalebela kudai Yanga ilitania tu kuwa ingemsajili Chama.

Uamuzi wa TFF wasubiriwa kuhusu suala hilo.

**marobarnabas@yahoo.com**
**0784 334 096**

# Waandishi watakiwa kuchukua tahadhari corona

**Na Romana Mallya**

SERIKALI ya Mapinduzi Zanzibar imetoa mwongozo kwa waandishi wa habari kwa kuwataka kujiepusha na mahojiano ya ana kwa ana ili kujiepusha na athari za virusi vya corona.

Vilevile, wahariri wametakiwa kuwapunguza waandishi wa habari kwenye vyumba vya habari kwa kadiri inavyowezekana.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa juzi na Mkurugenzi wa Idara ya Habari (Maelezo) Zanzibar, Dk. Juma Mohammed Salum, taasisi za serikali zimetakiwa kuwatumia Maofisa Habari kukusanya na kusambaza habari kupitia idara hiyo.

"Taasisi binafsi na wananchi kwa ujumla tunawaomba kuwasiliana na Maelezo mnapokuwa na taarifa ambazo mnahitaji ziwafikie wananchi. Waandishi wa habari mjikite zaidi kwenye habari kwa njia ya simu na mitandao zaidi," alisema.

Pia, Idara hiyo ya habari imetaka vyanzo vya habari na waandishi wa habari kujiepusha na mahojiano ya ana kwa ana nje ya studio.

"Mahojiano ya ndani ya studio tunawashauri kuwapo na umbali baina ya mtu na mtu. Kutumia kamera zisizo na rubani 'drone' ni bora zaidi katika matukio mbalimbali," alisema.



Mganga Mkuu wa mkoa wa Morogoro, Kusirye Ukio, akitoa mafunzo kwa askari wa Jeshi la Polisi mkoani humo juzi, kuhusu kujikinga na maambukizi ya virusi vya corona wawapo kazini. **PICHA: FRANK KAUNDULA**

# Vijana hatarini kupata maambukizi corona

**Na Daniel Limbe,** CHATO

LICHA ya kuendelea kuongezeka maambukizi ya virusi vya corona nchini, udhibiti wa tatizo hilo haujachukuliwa kwa baadhi ya vijana kutokana na kuchangia pombe kali katika chupa moja.

Pia, wanavuta sigara moja zaidi ya watu watatu bila kujali maambukizi ya virusi vya corona pamoja na magonjwa wengine.

Nipashe katika uchunguzi wake, imebaini baadhi ya vijana hao wilayani Chato, mkoani Geita, wanaotumia kinywaji hicho na walipoulizwa kama wanatambua uwapo wa ugonjwa Covid -19 unaosababishwa na virusi vya corona na namna ya kujikinga, walionekana kutilia mkazo kunawa mikono kwa maji tiririka pamoja na sabuni, lakini suala la kuchangia chupa walidai hawana taarifa nalo.

Fredy Machumu, mkazi wa Kijiji cha Kalema wilayani hapa, alidai wataalamu wa afya wamesisitiza wananchi kunawa mikono na sabuni pamoja na kukaa umbali usiopungua mita moja na nusu, lakini suala la uvutaji sigara na unywaji pombe hawajaliwekea mkazo.

Stella Emanuel, mkazi wa kijiji cha Chato kati, alidai kuwa licha ya kutambua kuwa kuna ugonjwa hatari wa Covid -19 na kuambukiza kwa njia ya hewa na majimaji yatokayo mdomoni kwa mtu aliyeambukizwa ugonjwa huo, alidai umaskini wa wananchi ndio unaosababisha kuchangia pombe moja bila kuzingatia kanuni za afya kama inavyoshauriwa na wataalamu.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Wilaya ya Chato, Dk. Ligobeth Kalisa, alisema kitendo cha watu zaidi ya mmoja kuchangia chupa moja ni hatari kwa afya ya wanywaji. Aliwataka kujiepusha na tabia hiyo ikiwamo kuchangia sigara moja kwa kuwa hali hiyo inaweza kueneza kwa kasi ya maambukizi ya ugonjwa wa corona iwapo mmoja wao akiwa na ugonjwa huo hatari.

Alisisitiza jamii kunawa mikono kwa majisafi yanayotiririka pamoja na sabuni ili kuepuka maambukizi ya ma-

# Polisi waomba kuangaliwa dhidi ya maambukizi

**Na Frank kaundula,** MOROGORO

JESHI la Polisi mkoani Morogoro, limeonyesha wasiwasi wa kuwa na hatarini kukumbwa na maambukizi ya virusi vya corona kufuatia matukio mbalimbali yanayoripotiwa bila kujua chanzo cha matukio hayo.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Morogoro, Wilbroad Mutafungwa, alionyesha wasiwasi huo wakati jeshi hilo likipokea mafunzo ya kujikinga na maambikizi ya corona wawapo kazini.

Alisema askari ndio watu wa kwanza kufika katika matukio mbalimbali husasani vifo vinavyotokea mitaani bila kujua chanzo cha vifo hivyo.

"Sisi askari tulikuwa hatuna elimu ya kutambua mgonjwa wa corona, lakini hata zinapotolewa taarifa ya mtu anayeshukiwa na maradhi sisi jeshi la polisi ndio tunakuwa mstari wa mbele kufika katika tukio," alisema Kamanda Mtafungwa.

Alisema kumekuwapo na ripoti za matukio mbalimbali ya vitendo vya kihalifu ikiwamo vifo na askari wa polisi ndio watu wa kwanza kufika eneo hilo bila kujali sababu ya kifo hicho.

"Nadhani wakati umefika wizara kutuangalia sisi jeshi la polisi katika ugawaji wa vifaa kinga sio tu kwa kuwaangalia wahudumu wa afya, hata sisi tupo hatarini sana kutokana na umuhimu wetu," alisema.

Mganga Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Kusirye Ukio, alisema tayari utaratibu wa ugawaji wa vifaa kinga kwa taasisi ambazo zinahusika moja kwa moja na kuwahudumia wananchi umeshawekwa baada vifaa hivyo kukabidhiwa mkoani.

Alifafanua kuwa serikali imeshapokea vifaa kutoka kwa wadau na wafadhili mbalimbali ili kusaidia wataalamu kujikinga wakati wa utoaji huduma na kwa sasa wanapaswa kuendelea kutumia vifaa elekezi katika kujikinga. "Tunatarajia wadau kutuchangia vifaa wiki ijayo pamoja na jitihada zetu za kila taasisi kupata vya kwao, kila kifaa tutakachokipata tutakipeleka sehemu muhimu, vinaweza visitoshe, lakini kitakuwa ni kianzio," alisema.

Dk. Ukio aliongeza kuwa, kwa sasa ndani ya Mkoa wa Morogoro hakuna mgonjwa aliyegundulika kuwa na maambukizi ya virusi vya corona ingawa kuna watu saba wanafuatiliwa na vipimo vyao vilishapelekwa maabara kuu kwa ajili ya uchunguzi zaidi.

Mtaalamu wa afya wa hospitali hiyo, Johanes John, aliwaomba askari hao kusimamia kikamilifu utekelezaji maagizo ya serikali ya kuwataka wananchi kunawa maji yanayotiririka na sabuni hasa katika maeneo ya mikusanyiko ikiwamo vituo vya mabasi na masoko.

"Hili suala sio la watu wa afya pekee, ukienda baadhi ya maeneo kama stendi ya Msamvu licha ya kuwapo kwa ndoo za maji, lakini watu wanapita bila kunawa na askari wetu wapo hawawachukulii hatua," alisema.

# Mbunge ataka uhakiki wa leseni za bodaboda, bajaji

MBUNGE wa Viti Maalum (Chadema), Zainab Mussa Bakar (pichani chini), ameitaka serikali kuhakiki leseni za bodaboda na bajaji kutokana na kuwa chanzo cha ajali za barabarani.

Kwa mujibu wa majibu ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, yaliyotolewa kwa swali la Mbunge huyo jana bungeni, uhakiki wa leseni za madereva unaofanywa na Jeshi la Polisi kupitia Kikosi cha Usalama Barabarani umesaidia kupunguza ajali za barabarani.

Ilieleza kuwa ajali hizo zinazosababishwa na bodaboda na bajaji kwa mwaka 2014 zilitokea jumla ya ajali 4,169 vifo 928 na majeruhi 3,884.

"Mwaka 2015 zilitokea jumla ya ajali 2,626 vifo 934 na majeruhi 2,370, takwimu hizi kwa kipindi cha miaka hiyo miwili kinaonyesha upungufu wa ajali 1,543 sawa na asilimia 37," ilisema.

Hata hivyo, ilisema kuna ongezeko la vifo sita sawa na asilimia 0.64 na upungufu wa majeruhi 1,514 sawa na asilimia 38.9.

Aidha, ilisema mwaka 2017 zilitokea ajali 1,459, vifo 728 na majeruhi 1,090 ambapo mwaka 2018 zilitokea 876, vifo 366 na majeruhi 694.

"Mlinganyo wa Takwimu hizi unaonyesha kwa kipindi hicho cha miaka miwili kinaonyesha kupungua kwa ajali 583 sawa na asilimia 39 kupungua kwa vifo 366 sawa na asilimia 50.2 upungufu wa majeruhi 396 sawa na asilimia 36.3," ilisema.

Kadhalika, ilisema kikosi hicho kinafanya operesheni za kuwakamata madereva wote wakiwamo wa bodaboda na bajaji wanaokiuka sheria na kanuni za usalama barabarani.

"Kikosi pia kinafanya ukaguzi wa leseni za madereva ili kuhakikisha kuwa leseni zote zimepatikana kwa kufuata utaratibu na kwa mujibu wa sheria kupitia mashine maalum kwa kuingiza namba ya leseni ni kutoa taarifa za uhalali wa leseni," taarifa ya wizara ilibainisha zaidi.



# Serikali: Ajali za mabasi zimepungua

BUNGE limeelezwa kuwa takwimu za ajali zilizosababishwa na mwendokasi kwa magari ya abiria yanayofanya safari za mikoani, zimeendelea kupungua kwa kiwango kikubwa.

Hayo yalibainishwa jana bungeni na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi katika majibu ya swali la Mbunge wa Viti Maalum (CUF), Rehema Migilla (pichani).

Katika swali lake, Mbunge huyo alisema serikali kupitia Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) imeanzisha mfumo wa kuratibu mwendo wa magari hususani mabasi ili kupunguza ajali kwa kufungwa ving'amuzi (VTS).

"Je, vifaa hivyo vimepunguza ajali kwa kiasi gani?"alihoji.

Katika majibu ya Wizara hiyo, ilielezwa kuwa VTS ni kifaa maalumu kinachofungwa kwenye gari ili kufuatilia mwendo wa gari barabarani, kuonyesha eneo na mahali.

"Kifaa hiki hakipunguzi mwendo wa gari bali hutoa ishara kwa dereva endapo atakuwa amezidi mwendo ulioidhinishwa kisheria na hivyo kumfanya dereva kupunguza mwendo ili kufikia spidi iliyopendekezwa na iliyoidhinishwa kisheria," ilisema taarifa ya wizara.

Hata hivyo, ilisema takwimu za ajali zilizosababishwa na mwendokasi kwa magari hayo zimepungua ambapo kwa mwaka 2016 kulikuwa na ajali 730 huku mwaka 2017 kulikuwa na ajali 509.

"Mwaka 2018 kulikuwa na ajali 364 na Mwaka 2019 zimetokea ajali 231, mfululizo huu wa upunguaji wa ajali unaonyesha mafanikio yanayopatikana kutokana na matumizi ya ving'amuzi kwenye mabasi ya abiria," taarifa hiyo iliongeza.



# Serikali haina kumbukumbu Barabara The Great North

WIZARA ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, imesema haina kumbukumbu zinazoonesha kuwa kuna barabara iliyopewa jina la 'The Great North Road' nchini.

Barabara hiyo inadaiwa ilipita njia ya Tunduru, Mbeya, Chunya, Itigi, Manyoni, Singida, Babati, Arusha hadi Namanga.

Wizara hiyo ilitoa majibu hayo bungeni jana ilipokuwa ikijibu swali la Mbunge wa Lupa (CCM), Victor Mwambalaswa (pichani).

Katika swali lake, Mbunge huyo alisema barabara hiyo ilipita kwenye maeneo hayo.

"Je, ni sababu zipi zimefanya Serikali kubadili njia hiyo kupitia Tangazo la Serikali(GN) na kuweka Mbeya, Iringa, Dodoma, Babati, Arusha na Namanga?" alihoji Mwambalaswa.

Katika majibu ya Wizara hiyo, ilisema haina kumbukumbu zinazoonesha barabara iliyopewa jina hilo.

"Barabara Kuu ya kaskazini (The Great North Road) inaanzia Cape Town nchini Afrika Kusini na kupita Botswana, Zimbabwe, Zambia, Tanzania, Kenya, Ethiopia, Sudan na kuishia Cairo nchini Misri (kilomita 10,288)," ilisema.

Kwa upande wa Tanzania, ilisema barabara hiyo inapita katika mikoa ya Songwe, Mbeya, Njombe, Iringa, Dodoma, Manyara na Arusha.

"Kwa mujibu wa "The Highway Ordinance Cap. 167, First Schedule, Main Road G.N. No. 471 ya mwaka 1962, Barabara Kuu ya Kaskazini nchini inapita Tunduma - Mbeya - Iringa - Dodoma - Babati - Arusha hadi Namanga na ina urefu wa kilometa 1,222,"ilisema.



Aidha, kwa mujibu wa Sheria ya zamani ya barabara (The Highway Ordinance Cap. 167) ya mwaka 1932, Barabara Kuu ya Kaskazini inapita katika maeneo hayo.




**Na Augusta Njoji,** DODOMA



## HABARI DODOMA

# Dodoma kutoa fomu maombi ya biashara bure

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

HALMASHAURI ya Jiji la Dodoma, itaanza kutoa bure fomu za maombi ya maeneo ya kufanyia biashara katika miradi mitatu ya kimkakati kwa wakazi wa jiji hilo pamoja na maeneo mengine nchini.

Miradi hiyo ni wa stendi ya mabasi ya kwenda mikoani, Soko Kuu la Ndugai pamoja na kituo cha mapumziko cha Changangali park.

Akizungumza na waandishi wa habari jiji hapa, Mkurugenzi Mtendaji wa Jiji la Dodoma, Godwin Kunambi, alisema eneo la stendi lina heka 60, wakati sokoni ni ekari 27 ambazo zinawatosha watu wengi.

Kunambi alisema kuwa eneo la stendi lina uwezo wa kutosheleza wafanyabiashara 700, na soko kuu la Ndugani wafanyabiashara 300.

Alisema wameamua kufanya hivyo kwa ajili ya kutoa nafasi kwa wakazi na wengine ambao sio wakazi wa Dodoma kuomba nafasi ya kupata maeneo hayo ya biashara.

"Wale waliolipa Sh. 20, 000 za awali fedha zao zitarudishwa, tunaanza kutoa bure," alisema Kunambi.

Alisema wameamua kuweka utaratibu wa kufanya maombi kwa njia ya mtandao ili kuepuka msongamano na maambukizi ya virusi vya corona.

Alisema watu ni wengi ila serikali inajitahidi kufanya kila kitu kwa njia ya mtandao na hakuna sababu ya wananchi kwenda ofisini na kusababisha msongamano. Alisema pia wameweka kila mahali vitakasa mikono kwa ajili ya watu kunawa kabla ya kuingia eneo la soko ili kupata mahitaji yao ya kila siku.

Kadhalika, alisema wakazi wa Dodoma wasiwe na wasiwasi kwa sababu halmashauri iko imara na inaendelea kuwakinga wananchi wake na ugonjwa wa huo.

Pia hakutakuwa na upendeleo katika ugawaji wa maeneo hayo.

Akitoa ufafanuzi kwa upande wa machinga, Kunambi alisema wasiombe kwa njia ya mtandao bali wamewatengea maeneo katika stendi na soko la Ndugai huku wakiwa na vitambulisho vya jiji.

# Wakulima wawezeshwa mbegu bora mtama

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

WAKULIMA 1,462 wa zao la mtama nchini, wamewezeshwa mbegu bora kwa ajili ya kutengenezea moja kati ya bia zinazozalishwa na Kampuni ya Tanzania (TBL).

Hayo yalielezwa juzi na Meneja Kilimo wa TBL, Joel Msechu, wakati alipotembelea mashamba ya mfano katika Kituo cha Utafiti wa Mazao (Tari), Hombolo nje kidogo ya Jiji la Dodoma.

Msechu alisema idadi hiyo ya wakulima nchini imewezeshwa mbegu bora za kilimo cha mtama katika msimu wa mwaka huu kwa lengo la viwanda vya kampuni hiyo kuzalisha aina ya bia inayotengenezwa nchini.

Alisema katika idadi hiyo wakulima 1,398 wapo katika Wilaya ya Kongwa na wamewezeshwa mbegu hizo kwa lengo la kujikwamua kiuchumi.

Alibainisha kuwa lengo la TBL ni kushirikiana na vituo vya utafiti vya Tari nchini kutafiti mbegu bora ya mtama ambayo itatumiwa na wakulima kwenye mikoa mbalimbali nchini. Aliitaja baadhi ya mikoa waliyoanza nayo katika uzalishaji huo wa mbegu bora kuwa ni Dodoma, Singida, Manyara na Tabora na mategemeo ni kuendelea na mikoa mingine katika msimu ujao wa kilimo wa 2020/2021.

Msechu alisema kupitia utafiti huo wanategemea idadi ya wakulima wa mtama itaongezeka kwa sababu watakuwa na uhakika wa mbegu ya kilimo inayofaa katika maeneo yao na soko la uhakika kwa mtama wote utakaozalishwa.

Alisema viwanda vyao vinahitaji mtama zaidi ta tani 15,000 kwenye viwanda vyao vinne vilivyopo nchini, hivyo wakulima wachangamkie kilimo hicho ili kuinua uchumi wao. Alivitaja viwanda vya TBL vilivyopo nchini vinavyohitaji mtama huo kwa ajili ya kuzalisha bia kuwa ni Dar es Salaam, Mwanza, Mbeya na Arusha.

Alisema lengo lao ni kuhakikisha wakulima wanauza mtama wote unaozalishwa kwenye maeneo hayo yaliyo jirani na kanda hizo na mkataba ni kuwa TBL wanawahakikishia kuwa watanunua mazao hayo. Alisema mbegu hiyo itakayozalisha kwenye mashamba hayo ya mifano itapelekwa kugawiwa kwa wakulima ili wapande kwenye mashamba yao msimu ujao wa kilimo.

Kwa upande wake, Meneja wa Tari, Hombolo Dodoma, Dk. Lameck Makoye, alisema TBL waliingia mkataba wa Tari kwa lengo la kuzalisha mbegu bora.

Dk. Makoye alisema, utafiti umebaini kuwa mbegu ya mtama aina ya masia inafaa kwa uazalishaji wa bia inayotengenezwa na kampuni hiyo na kuwataka wakulima wachangamkie.

Vile vile, alisema katika mkataba wao, Tari wanajukumu la kuhakikisha wanatoa elimu kwa wakulima wanaofika kwenye mashamba hayo ya mfano na kuwaelimisha namna ya kutumia mbolea. Pia alisema mkulima akizingatia kanuni bora za kilimo anazoshauriwa, atakuwa na uwezo wa kuvuna mtama kuanzia tani tatu hadi tatu na nusu kwa ekari moja.



Mwenyekiti wa Halmashauri ya Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA), wilaya ya Dodoma Mjini, Ustadhi Bashuru Hussein, akizungumza na Mashekhe na Maimamu wa misikiti na walimu wa madrassa, alipokuwa akitoa elimu ya kujilinda na maambukizi ya ugonjwa wa corona, jana. **PICHA PETER MKWAVILA**

# Kanisa laomba vilabu vya pombe kufungwa

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

KATIBU wa Kanisa la Aglikana Tanzania Dayosisi ya Kati (DCT), John Ntandu, ameiomba serikali kufunga vilabu vya pombe, baa na michezo ya 'pool' ilizopo vijijini kutokana na kuleta mikusanyiko inayoweza kusababisha kuwapo kwa maambukizi ya corona.

Ntandu alisema kama serikali ilivyoamuru vyuo, shule za sekondari, msingi na awali na maeneo mengine kufungwa kutokana na hofu ya kuwapo maambukizi ya ugonjwa huo, pia iangalie kwa upande wa vijijini ambako bado kuna mikusanyiko hiyo.


Ushauri huo aliutoa wakati akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa kutokana na kubainika kuwa baadhi ya vijiji kuwapo na vilabu vya pombe za kienyeji na baa zinazoleta mikusanyiko ya watu.

"Huko vijijini bado ugonjwa huu wa corona elimu haijawafikia watu kwa kiasi kikubwa kama mijini, hii ni kutokana na kuwapo kwa mikusanyiko kama vile ya kwenye vilabu vya pombe za kienyeji, baa na michezo ya pool," alisema.

Alisema pamoja na juhudi kubwa zinazofanywa na serikali mijini za kuwafanya wananchi kufuata kanuni na utaratibu wa kuepukana na ugonjwa huo, kwa huko vijijini utaratibu huo ni wachache wanaotekeleza.

Alisema pia bado kuna vijiwe vinavyokusanya vijana ambavyo ni hatari kwa kusababisha maambukizi kwenye mikusanyiko hiyo ambayo haina tija kwa kipindi kama hiki ambacho serikali imezuia. Katika hatua nyingine Katibu huyo pia ameiomba serikali, mashirika ya umma, watu binafsi na wataalamu wa afya, kuwakumbuka watu wenye ugonjwa wa ukoma waishio vijijini kwa kuwapatia vifaa na elimu ili waweze kujihami na maambukizi ya corona.

Alisema, bado kuna kundi la wagonjwa wa ukoma vijijini wanaohitaji msaada ya karibu kutokana na wengi wao kutokuwa na uwezo. "Kila mwenye ulemavu ana changamoto zake, lakini kwa hawa wenzetu wenye ugonjwa wa ukoma wanatakiwa kusaidiwa kwa ukaribu katika kipindi hiki cha uwapo wa ugonjwa huo kama vile elimu na vifaa ili waweze kujilinda na ugonjwa huo wa corona," alisema.





Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja, Hassan Khatib, akikagua ndoo za kuweka maji kwa ajili ya kuosha mikono, katika eneo la biashara la Sateni, Mjini Unguja jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Z'bar kuanza matumizi risiti kielektroniki

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar, imesema ipo katika hatua za mwisho za kufanikisha utumiaji na utoaji wa risiti za kielektroniki kwa ajili ya ukusanyaji wa mapato ya serikali.

Waziri wa Fedha na Mipango, Balozi Mohamed Ramia Abdiwawa, alisema hayo wakati akiwasilisha ripoti ya utekelezaji wa maagizo ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali (PAC), kwa mwaka wa 2019-2020. Alisema serikali imechukua muda mrefu kukamilisha mchakato wa risiti hizo ikiwamo kuweka mfumo mzuri ambao utafanya kazi zake kwa uhakika na kuleta mafanikio.

"Serikali ipo katika hatua za mwisho za kukamilisha mpango wa utumiaji na utoaji wa risiti za kielektroniki kwa ajili ya ukusanyaji wa mapato na kuongeza kupambana na watu ambao wanakwepa kutoa risiti na hivyo kuikosesha serikali mapato yake," alisema

Balozi Ramia, alisema Wizara ya Fedha na Mipango imepata mafanikio makubwa baada ya kuweka na kuimarisha mifumo ya usimamizi wa mapato na matumizi yake. Aliyataja mafanikio hayo ikiwamo kudhibiti uvujaji wa mapato kutokana na kuimarisha mifumo yake ya ukusanyaji kwa kutumia njia za kibenki na mitandao ya simu za mikononi.

"Matumizi ya fedha za serikali ikiwamo ukusanyaji wa mapato na malipo yote kwa asilimia 90 yanafanyika kwa njia ya kibenki na tumefanya hivyo kwa ajili ya kudhibiti uvujaji wa fedha kuingia katika mikono ya wafanyakazi wasiokuwa waaminifu," alisema.

Akitoa maoni ya kamati hiyo, Makamu Mwenyekiti Shaibu Khamis Ali, aliitaka Mamlaka ya Kupambana na Rushwa na Uhujumu wa Uchumi Zanzibar (ZAECA), kufanya uchunguzi wa baadhi ya taasisi za serikali ambazo zimebainika kufanya matumizi mabaya yanayokwenda kinyume na sheria za fedha za serikali.

Alitaka Ofisi ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali kufanya ukaguzi wa matumizi ya fedha na mapato ya baadhi ya mashirika ya serikali ambayo hayajakaguliwa kwa muda mrefu.

"Kamati yetu ya kuchunguza fedha za serikali tumebaini kwamba bado yapo mashirika makubwa ya serikali na baadhi ya taasisi hazijakaguliwa matumizi yake ya fedha na mapato...hiyo ni kasoro kubwa katika masuala ya fedha," alisema.

# SMZ yatakiwa kutengeneza mpango kukabili athari kiuchumi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

KAMATI ya Bajeti ya Baraza la Wawakilishi, imeishauri serikali kutengeneza mpango madhubuti wa kukabiliana na athari za kiuchumi zinazosababishwa na kasi ya ugonjwa wa corona.

Hayo yalisemwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti ya Baraza la Wawakilishi, Dk. Mohamed Said Dimwa, wakati akichangia maagizo ya ripoti ya bajeti kwa Wizara ya Fedha na Mipango ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka 2019-2020.

Dk. Dimwa alisema uchumi wa dunia upo katika hatari kubwa ya kuyumba na kuporomoka kutokana na baadhi ya nchi kupiga marufuku mikusanyiko pamoja na kuingia wageni ikiwamo watalii na hivyo kukosa mapato yanayotegemewa kutoka katika sekta mbalimbali.

Alisema kamati ya bajeti inaishauri Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kufanya mawasiliano na Serikali ya Jamhuri ya Muungano kupitia Kamati ya Kitaifa ya Mawaziri ili kuweka mikakati ya kitaifa kupambana na janga la ugonjwa wa corona lisiathiri zaidi uchumi wa taifa.

Alisema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Muungano zishirikiane kutafuta usaidizi wa taasisi za kifedha ikiwamo Benki ya Dunia na Shirika la Fedha la Kimataifa kwa kuwa taasisi hizo huweka bajeti kwa ajili ya kukabiliana na changamoto za kiuchumi.

Aliitaka serikali kuomba kupewa nafuu ya madeni yake kwa kuondolewa au kupunguziwa riba katika kipindi hiki ambacho taifa linapambana na ugonjwa wa corona ambao miongoni mwa athari zake ni za kiuchumi.

"Huo ndio ushauri wetu kamati ya bajeti...ushirikiano wa pamoja unahitajika katika suala la kifedha na uchumi kukabiliana na janga la ugonjwa wa corona," alisema.

Asilimia 80 ya fedha za kigeni za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zinatoka katika sekta ya utalii ikijumuisha hoteli za kitalii zilizopo katika mwambao wa pwani ya visiwa hivyo na eneo la Mji Mkongwe.

# Faini papo kwa papo kuwakabili madereva

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar, imesema ipo katika hatua za mwisho za kutayarisha adhabu za faini za 'papo kwa papo' ikiwa ni moja ya hatua ya kupambana na kudhibiti ajali nyingi za barabarani ambazo baadhi yake husababishwa na madereva kwa uzembe.

Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji, Dk. Sira Umbwa Mamboya, alisema hayo wakati akitoa ufafanuzi na kujibu kwa baadhi ya hoja za wajumbe wa Baraza la Wawakilishi waliochangia ripoti ya Kamati ya Ardhi na Mawasiliano kwa mwaka 2019-2020.

Dk. Mamboya alisema ajali za barabara zimekuwa zikiongezeka na nyingi zikisababisha vifo vya wananchi wasiokuwa na hatia na baadhi yake kuwasababisha ulemavu wa kudumu.

Alisema mchakato wa faini za papo kwa papo umeanza ikiwamo kutayarisha kanuni kwa kuwasiliana na taasisi mbali bali ikiwamo Jeshi la Polisi ambao watakuwa wasimamizi wakubwa wa sheria na adhabu hizo.

"Mheshimiwa Spika, napenda kulijulisha Baraza la Wawakilishi kwamba, tupo katika hatua nzuri ya kutayarisha faini za adhabu za 'papo kwa papo' kwa madereva wanaofanya makosa ya kizembe ambayo husababisha ajali na kutishia maisha ya watu wetu," alisema.

Akichangia taarifa ya kamati hiyo, Mwakilishi wa Jimbo la Magomeni, Rashid Makame Shamsi, alisema faini za papo kwa papo zinaweza kuwa suluhisho kwa kiasi kikubwa katika kupambana na kupunguza ajali za barabarani, Zanzibar.

Alisema takwimu zinazotolewa na Mtakwimu Mkuu wa Serikali kuhusu ajali za barabarani zinatisha na zinaonyesha kuwapo kwa mikakati ya ziada kukabiliana na tatizo hilo.

"Sisi Wawakilishi tumefurahishwa na taarifa ya kuja kwa mpango wa faini za papo kwa papo kwa madereva wetu ikiwa moja ya hatua za kupambana na ajali za barabarani ambazo zinaongoza kwa vifo vya wananchi kupata ulemavu baada ya kujeruhiwa," alisema.



## RIHANNA TAFUTA RADHI YA BABA UK.14

Nipashe MWANGA WA JAMII
BT
JUMAMOSI APRILI 18, 2020



### VITA KALI

# Zuchu, Ibraah Tz watoana jasho

SASA ni dhahiri kuna ushindani kati ya wasanii wa muziki wa Bongo Fleva, Harmonize na Diamond, baada ya lebo wanazoziongoza kutangaza wasanii wapya.

Wakati Msanii Diamond wiki iliyopita alimtangaza msanii mpya Zuchu, Harmonize kwa upande wake mapema wiki hii alimtambulisha Ibraah TZ, kuwa mwanamuziki ndani ya lebo ya Konde Gang. Katika kile kinachoonekana kwamba pande hizo zinafanya jambo kwa utafiti, wasanii hao wote wanaimba nyimbo zenye mahadhi ya taratibu zinazobeba hisia kali za kimahaba.

Baadhi ya watu wanadai kutambulishwa kwa wasanii hao ndio mwanzo ya vita kali ya kisanii kati ya lebo hizo mbili kwa kuwashindanisha wasanii katika soko.

BASI SAWA

# Mzee wa Bwax kwani kujipodoa na singeli tofauti?

MSANII wa singeli, Mzee wa Bwax, amewatahadharisha wanaoimba muziki huo kuacha kiki zitakazowaua kisanii na kwamba masuala ya kujipaka vipodozi au kujichubua wawaachie Bongo Fleva.

Akizungumza na eNewz, Mzee wa Bwax, alisema mashabiki wa singeli hawataki mambo makubwa, wao wanachojali uzuri na ubora wa muziki pekee.

"Nashangaa Dulla anapaka poda, kiki za aina hiyo na zile za kujiua waachie Bongo Fleva. Mimi napiga muziki kwa ajili ya mashabiki wangu wananikubali sana," amesema.





# KUMEKUCHA Billnass, Nandy kuwajibu kivitendo

WAPO wanaotamani kuwaona wasanii wa muziki wa Bongo Fleva, Billnass na Nady, wanafunga ndoa haraka.

Watu wengi walitoa maoni baada ya wasanii hao kuvishana pete ya uchumba, waliwashauri kuacha tabia za watu wengine maarufu ambao baada ya hatua hiyo wanaishia kuachana.

Hata hivyo, kupitia ukurasa wake wa Instagram, Billnass amewajibu kiaina kwa kueleza kwamba amewasikia, na atafuata ushauri wao.

"Pili Nitumie muda huu kushukuru kwa salamu za birthday na pongezi za Engagement, sms, simu, post , comment, ushauri ni vingi sana nilitamani kumuonesha kila Mmoja how Much I appreciate lakini mimi pia ni binadamu, nisingeweza kumridhisha kila mmoja, ila niseme tu nawapenda sana," ameandika.

# Baba levo acha kumnanga Msechu

MWANAMUZIKI na diwani wa Mwanga Kaskazini mkoani Kigoma, Baba Levo, amesema anachukia umbo la msanii mwenzake, Peter Msechu, na wakati mwingine huwa anamshambulia kwa maneno awe mwembamba kama Vanessa Mdee.

Akizungungumza na EATV, Baba Levo, amesema huwa anajisikia raha pale anapompakia maneno Msechu na lengo lake ni kumtaka akonde na kumpa mawazo.

"Najisikia raha ninapomshambulia Peter Msechu, lengo la kumshambulia huwa nataka akonde na nimpe mawazo ili awe na mwili flani hivi kama Vanessa Mdee, nataka hata akitembea awe sawa na Vanessa, ila siwezi nikamtania hadi kumvunjia mipaka yake kwa mfano kufika hadi kwa wazazi" amesema Baba Levo .







# Siri iliyojificha Kings Records

KUJIENGUA kwa wanamuziki wawili katika lebo ya Kings Records, kumeibua mambo mapya, baada ya watu kuanza kutilia shaka na kudai kuna mkono wa mtu.

Wasanii ambao wametangaza kujitoa ndani ya lebo hiyo ni Killy na Cheed, ambao kupitia mtandao wa Instagram kila mmoja aliandika ujumbe wa kuondoka katika lebo hiyo.

Hata hivyo, wakizungumza na redio moja walisema wamefanya hivyo kutokana na wazazi wao kuwashauri kufanya hivyo.

Katika maelezo yao, Cheed alisema mama yake alimshauri kuondoka si mara nmoja, lakini alishindwa kutekeleza ushauri wake.

"Unajua hakuna mtu aliyetushawishi, jambo hili tumelifanya baada ya wazazi wetu kukataa tuwe huko, sisi kama watoto tumeona bora tuufuate," amesema.

Baada ya kutoa sababu hizo, baadhi ya mashabiki wa muziki walijitokeza na kupinga sababu hizo walizotoa na kusema wasanii hao wapo mbele ya watu waliowashawishi.

"Wasanii hawa bado wachanga, hawakufikia muda wa kujitegemea kama wanavyodai na hata wakisema mama zao wamewashauri, hilo haliwezekani lazima kuna watu wamekaa nyuma yao," alisema Shukuru Saidi.

Katika ujumbe wao za awali, Killy, aliandika maneno haya "Leo hii napenda kutamka kuwa mimi sio tena msanii wa Kings Music Records, nimeamua hili kwa akili yangu timamu kabisa, bila kushawishiwa na mtu yeyote na sijatumia kilevi chochote kile ni maamuzi yangu binafsi kwa ajili ya muendelezo wa mziki wangu, namshukuru sana Alikiba kwa kila alichonifanyia na kujitolea kwa ajili ya mziki wangu, na sitoacha kumshukuru siku zote za maisha yangu naumia ila sina budi" ameandika Killy.

Hata hivyo, Kiba amesema hana kinyongo na wasanii hao na kueleza kwamba anawakia kila la heri katika safari yao ya kimuziki.



# Ngoma 5 mpya kali za Machi

**Na Adam Fungamwango**

HUWEZI kuamini, lakini ndiyo ukweli wenyewe kuwa, mwezi uliopita, yaani mwezi Machi, wasanii wa bongo fleva ni kama vile walikuwa wanafanya mashindano ya kutoa ngoma mpya.

Ni kama vile wanashindana kulala studio, ukiamka huyu katoa ngoma, yule kajibu kwa kutoa ngoma, ili mradi tu mwezi Machi umetisha kwa wasanii wa bongo kutoa ngoma, tena si za kitoto. Hizi ni ngoma tano kali zilizotolewa mwezi Machi na kukwa muda mfupi tu zimepokelewa vema na mashabiki wa muziki huyo.

**BEN POL FT GODLUCK GOZBERT-MAMA**

Mwanzoni tu mwa mwezi Machi, tarehe saba, msanii Ben Pol, akiwa amemchukua msanii mwenzake Godluck Gozbeth alitoa ngoma mmoja kali waliyoiita 'Mama'.

Ni ngoma inayoelezea jinsi mtoto anavyokubali kazi aliyoifanya mama yake tangu yupo tumboni, kumzaa, safari ya malezi, elimu, hadi kujua jema na baya na kuanza maisha yake.

**RAYVANNY-EX BOYFRIEND**

Siku moja baadaye, yaani Machi 8, baada ya kina, Ben Pol, kutoa ngoma yao, msanii Rayvanny naye akatoa ngoma yake kali ambayo ameipa jina la 'Ex Boyfriend, ikiwa na maana ya mpenzi wa kiume za zamani.

Hapo ni masuala ya mapenzi, hasa kwa watu ambao awali walikuwa wapenzi, lakini wakashindwa kuzuia hisia zao wakagombana na sasa mmoja anataka kumrudia mwenzake, lakini mwingine anagoma katakata. Ni moja kati ya ngoma kali za mwezi Machi.

**WHOZU FT DIRECTOR SHAIBUBUKU**

Hii ni ngoma yenye mahadhi ya singeli. Haina meseji sana, badala yake imejikita mno kwenye fani na si maudhui.

Ni ngoma inayochezeka pamoja na midundo yake, lakini uzuri zaidi wa ngoma hii uko kwenye video ambapo kuna akinadada wanatwimbilika kinoma.

Ngoma hii ilitoka Machi 9, na sasa ni gumzo mtaani.

Young Killer-So Sad

Msanii Young Killer naye hakukaa kimya. Machi 10, akatoa ngoma yake kali ambayo anaiita 'So Sad' na kuingia kwenye orodha ya wasanii waliotoa ngoma kali mwezi uliopita.

**MBOSSO-TAMBA**

Ngoma hii ambayo imetoka Machi 22, tayari ni gumzo kubwa mitaani kutokana na maudhui yake, pamoja na video yake iliyopangiliwa vema.

Pamoja kwamba imetoka Machi 22, lakini kwenye mtandao wa msanii huyo imeshatazamwa na watu zaidi ya milioni 2 mpaka sasa.



# Ananipwelepweta Penzi la mseto mchungu

**Na Adam Fungamwango**

NI kweli penzi halina macho, halina umri, rangi wala kabila. Penzi humea popote pale hata porini kama uyoga. Hata hivyo kuna vitu vya kutazama kwanza kabla ya kuingia mzima mzima kwenye mapenzi, vinginevyo unaweza kujikuta umetumbukia kwenye penzi na ndugu yako, au hata mzazi.

Kwenye filamu ya 'Ananipwelepweta' limetokea jambo kama hili la kuhuzunisha.

Mtunzi alikuwa anataka jamii ichukue tahadhari kabla hayajawakuta na wale yaliyowakuta, wawe mabalozi wazuri wa wenzao.

Imechezwa na wasanii wengi, lakini maarufu zaidi ni Riyama Ally na Slim Omari.

Imeanza kwa mzee Bungara na mkewe mama Somoe wakiishi kijijini maisha duni. Ni maisha yaliyomchosha mama Somoe na kuamua kutoroka kijijini kwenda mjini kutafuta maisha.

Akamtoroka mumewe mzee Bungara, akiongozana na mtoto wake wa kike Somoe.

Kijijini alimuacha mumewe na mtoto wa kiume, Mhagama. Akiwa mjini aliomba vibarua kwa mama lishe na kulala njiani.

Anagongwa na gari, lakini jamaa alikuwa msamaria mwema na kuamua kumpeleka hospitali, akimlipia pia matibabu hadi akapona. Jamaa alimchukua na kumpeleka nyumbani kwake. Huko akafanywa mke kwani jamaa hakuwa na mwenza, hivyo mama akaishi na binti yake Somoe.

Baada ya miaka kadhaa kupita, mama Somoe alibadilika na kutaka kurithi mali ya yote ya Simba, hivyo akamuua na kurithi mali yote. Miaka 20 baadaye Mhagama alimuaga baba yake kuwa anakwenda mjini kutafuta kazi.

Aliingia mjini na kama kawaida hakuna kwenye wakati mzuri, kwani aliishia kusukuma mkokoteni wa maji.

Moja kati ya wateja wake ni mama Somoe. Shetani akamuingia mama wa watu. Akamtamani na kumfanya kibenteni. Jambo hili lilimkasirisha mno Somoe, lakini mama yake alitumia cheo cha umama kumyamazisha na kumtisha binti yake. Kazi ikawa ni kuponda raha na kula maraha, hadi mama wa watu kitumbo ndi.

Mhagama akampigia simu baba yake kuwa mjini mambo yake ni poa, ana maisha mazuri, lakini pia ana mchumba anayetaka kumuoa.

Mzee anamtuma jirani yake, kijana Baraka, aende mjini kwa mwanaye, lakini alipofika alishangaa kuona kwenye nyumba hiyo watu wote ndani anawafahamu.




# Haa! Wizkid utapagawisha wenzako

WANAMUZIKI wa Nigeria, Zlatan, Poco Lee, Bella Shmurda na Q2, wamejikuta wakitumia mtandao wa Instagram kama jukwaa la muziki baada kuimba mbele ya Wizkid.

Wakiimba nyimbo ya Wizkid, wanamuziki hao walikonga nyoyo ya mashabiki waliokuwa wakifuatilia kupitia Instagram Live.

Wizkid alijikuta akisema anataka kuwa na nyumba maalum kama zawadi kwa wanamuziki hao.



## AY usichukie, labda kuna ukweli

MCHEKESHAJI kutoka Nigeria, AY Makun, ameamua kuonyesha penzi la nyuki, baada ya kumtetea mkewe kwamba umbo lake halikutengenezwa  bali ameumbwa na mola.

Mkewe Mabel, amelalamikiwa na mashabiki wake kuwa amefanyiwa upasuaji wa kurekebisha umbo lake.

"Hapa hakuna kitu kinachoendelea kuhusu mke wangu, wapo wanaosema kwamba umbo lake ni feki na blabla zingine.Naona wanaimba wimbo tu," amesema.

## Adeniyi ulijuaje corona inavyoimarisha ndoa?

MWIGIZAJI kutoka Nollywood, Adeniyi Johnson, ameamua kutoboa siri baada ya kusema sasa wake wenye utata wanaweza kuishi na waume zao kwa upendo katika kipindi hiki cha COVID 19.

Akitumia ukurasa wake wa Instagram, amesema baadhi ya wanawake hawakuwa na tabia ya kutulia nyumbani, lakini sasa wanaweza kuishi na waume zao bila ya matatizo.

Kulingana na Johnson, kuna wakati wanawake wamekuwa wakiwaweka roho juu wanaume na kuhatarisha ndoa zao, lakini wakati huu wa zuio la kutotoka nje mapenzi yamekuwa moto.





## Peter ni kweli haya unayosema?

MWANAMUZIKI nyota wa Nigeria, Peter Okoye, ameweka wazi kwamba alipokutana na mke wake Lola Omotayo, akiwa na miaka 18 alichanganyikiwa.

Peter ambaye alikuwa mmoja wa wanamuziki pacha wa Psquare, alitumia ukurasa wake wa Instagram live akiwaambia mashabiki wake kuwa alipomuona alidhani amekutana na dhahabu

"Nilipomuona mke wangu akiwa na miaka 18, nilikuwa kama mchimbaji akitafuta dhahabu nikiwa nimechanganyikiwa," amesema.

## Rihanna tafuta radhi ya baba

STAA wa muziki wa Marekani, Rihanna, amethibitisha kuwa baba yake ameambukizwa ugonjwa wa corona.

Mwanamuziki huyo alisema amejiandaa na tatizo lolote baada ya kununua kifaa cha kusaidia kupumua kwa jili ya baba yake endapo hali yake itakuwa mbaya.

Baba yake huyo Ronald, alikuwa katika karantini ya siku 14 na baada ya kufanyiwa vipimo ameamua kujitenga huku akiangalia afya yake.



MAKALA



Mkurugenzi wa Shirika la Afya Ulimwengini (WHO) Tedros Adhanom Ghebreyesus

# Dunia yagawanyika Marekani kujiondoa WHO

**Na mwandishi Wetu**

DUNIA imegawanyika kuhusu hatma ya Shirika la Afya Duniani (WHO), kufuatia uamuzi uliochukuliwa na Rais wa Marekani, Donald Trump, kuondoa ufadhili.

Rais Donald Trump, Jumanne aliagiza kusitishwa kwa ufadhili wa Marekani katika Shirika la Afya Duniani wakati linakabiliana na janga la virusi vya corona lililokumba ulimwengu.

Rais Trump, amesema hatua hiyo inatekelezwa kutokana na kulituhumu shirika hilo kutotimiza majukumu yake ipasavyo katika kukabiliana na ugonjwa wa covid-19, na kutosema ukweli kuhusu maambukizi hayo.

"WHO ingekuwa imefanya kazi yake ya kutuma wataalamu wa kitabibu nchini China ili kutathmini hali ilivyo, ugonjwa ungeweza kudhibitiwa na kutokea kwa idadi ndogo ya vifo," Trump alisema.

Hata hivyo, kiongozi huyo anaituhumu WHO kuipendelea China ambayo ndio chimbuko la janga la corona.

Baada ya tangazo hilo, nchi mbalimbali zimejitokeza kulitetea shirika hilo, pamoja na kuitaka Marekani kuacha mpango huo kwani inaweza kudhoofisha vita dhisi ya ugonjwa huo.

**WHO INAPATAJE FEDHA?**

Shirika hilo lililoundwa mwaka 1948, kama sehemu ya mfumo wa Umoja wa Mataifa, kazi yake kubwa ni kukuza afya, kuhakikisha dunia inakuwa salama na kuhudumia wale walio katika hatari zaidi ya magonjwa.

Taasisi hiyo, ambayo makao makuu yake yako Geneva, Uswisi, imekuwa na bajeti ya dola bilioni 5.6 kwa kipindi cha miaka miwili inayoanzia 2018 hadi 2019.

Vyanzo vya mapato yake ni michango ya lazima kutoka nchi zote 194 ambazo ni wanachama.

Michango hii inatofautiana kwa kila nchi kutokana na uchumi wake na idadi ya watu,

Katika bajeti hiyo, ufadhili ulijumuisha karibia dola milioni 950 za Marekani.

Mapato mengine yanatokana na ufadhili wa kujitolea. Hii ni pale nchi moja inapoamua kuchangia kwa suala maalum, kama vile chanjo, afya ya wanawake au ukabilianaji na matumizi ya tumbaku.

Katika bajeti hiyo zilikuwa dola bilioni 4.3.

**CHANZO CHA TATIZO**

Kwa mujibu wa Jack Chow, aliyekuwa balozi wa Marekani katika kukabiliana na ukimwi na aliyekuwa Naibu Mkurugenzi wa WHO, anasema katika miaka ya hivi ya karibu shirika hilo limekuwa tegemezi kupata rasilimali zake.

"Hali hii inasababisha matatizo kwa sababu wafadhili ndio wanaoandaa ajenda zitakazofuatwa na shirika hilo badala ya kufanya uamuzi wao kwa kuzingatia taaluma," Chow ameiambia BBC.

Marekani imekuwa mfadhili mkubwa wa WHO kwa kutoa mchango wa miaka miwili wa dola milioni 893, tayari imetoa dola milioni 553 kufikia robo ya nne ya 2019. Fedha hizo sawa na asilimia 14.57, katika bajeti hiyo.

China imechangia dola milioni 86, ambayo tayari imetoa dola milioni 7.9. Ikiwa ni sawa na asilimia 0.21.

Rais Trump anatumia nafasi hiyo, kuweka ushawishi wake kwa kuishtumu WHO kushindwa kuzungumza na serikali ya China kuhusu uchangiaji wao na chimbuko la mlipuko wa sasa wa virusi vya corona.

Nafasi ya pili kuichangia taasisi hiyo, ni shirika la Bill and Melinda Gates Foundation, ambalo limeahidi kutoa dola milioni 530, tayari imetoa dola milioni 367.

Hata hivyo, shirika la Gates liliungana na nchi za Kiafrika na Ulaya kukosoa amri ya Trump ya kusitisha uchangia wake kwa WHO.

Shirika la GAVI, linaloshughulika na upatikanaji wa chanjo kwa nchi 73 katika maeneo ya kaskazini kote duniani, inashika nafasi ya tatu inatoa dola milioni 316.

Nchi zingine zinazochangia kwa wingi ni Uingereza imewasilisha dola milioni 294, Brazil (35.5), Mexico (13.7) na Argentina (8.5).

**ATHARI YAKE NINI?**

Ikiwa Marekani itafanikiwa kuzuia mchango wake, WHO itakuwa na changamoto kubwa kiasi ambacho baadhi ya majukumu kuyafuta.

"Uamuzi wa Trump kusitisha ufadhili kwa WHO utakuwa na athari kubwa," anaongeza kusema Dk. Jack Chow katika mahojiano na BBC Mundo.

Anaongeza wasiwasi wake "Lengo kuu la WHO ni kuzuia kusambaratika kwa mifumo ya afya ambao ni dhaifu duniani. Washauri wa WHO wanashirikiana na idara za afya, madaktari, wafanyakazi wa afya kuwasaidia kutoa huduma bora kwa wagonjwa,"

Anasema hatua ya Trump huenda ikahatarisha miradi mingi, ikiwamo kufutwa kazi kwa washauri wengi wa WHO kutoka nchi mbalimbali duniani.Watu wengi wa maeneo kama vile Amerika ya Kusini huenda wakawa hatarini sio tu kwasababu ya covid- 19, lakini hata kwa magonjwa mengine mengi kama kifua kikuu na malaria.

Kulingana na takwimu za WHO zilizotolewa hivi karibuni, michango ya Marekani iliyotolewa kwa miaka miwili imesaidia nchi 22 mashariki ya Mediterranean.

Eneo hilo limepokea dola milioni 201, sawa na asilimia 36 ya pesa zilizotolewa na Marekani.

Eneo la pili lenye kupokea kiwango cha juu cha pesa hizo ni Afrika, ambayo inajumuisha nchi 47 ambazo zimepokea dola milioni 151.

Makao makuu ya WHO, inapokea dola milioni 101 kutoka Marekani, kiasi hicho kinatumika kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli zake na kampeni kadhaa za masuala ya afya.

Ni asilimia kidogo ya ufadhili wa Marekani wa dola 280,000 zimetumika kufadhili shughuli za WHO kwa nchi za Amerika ya Kusini na Caribbean.

Sehemu hiyo ni baadhi tu ya maeneo yanayopata fedha zilizotengwa, lakini kuna mambo mengine kama kukabiliana na Ukimwi na homa ya ini. Pia inatumika uzuiaji na udhibiti wa kutokea kwa majanga pamoja na pesa za kukabiliana na magonjwa ya kitropiki hadi afya ya uzazi.

Chow anakubaliana na maoni kwamba, shirika hilo linahitaji kufanyiwa mabadiliko na kuimarishwa kama linataka kufanya kazi kwa kujitegemea.

**BBC**

MAKALA

# Mafuriko yalivyobadilisha maisha Kusini



Mitumbwi ikitumika kuwaokoa watu waliozingirwa na maji wilayani Rufiji.

**Na Moshi Lusonzo**

MIKOA ya kusini mwa Tanzania imejikuta ikikabiliwa na maafa ya mafuriko ambayo hayajawahi kutokea katika miongo minne.

Mikoa ya Pwani, Lindi na Mtwara ni baadhi ya maeneo yaliyoathiriwa na mvua zinazoendelea kunyesha nchini na kusababisha mito na mabonde kujaa maji.

Kwa wale wanaosafiri kwenda mikoa hiyo, mtakubaliana na balaa hili, kutokana na macho yao kupambana na picha halisi ya athari zilizoletwa na mvua hizo.

> **"Maji yakiendelea kuwa kama hivi mashambani kuna wasiwasi wa kuwepo kwa njaa, maoni yangu ni kuangalia namna ya kuwasaidia wananchi hawa walioathirika,"**

Kwa mfano, unapoanza kukutana na bonde la mto rufiji, utaona jinsi uoto wa asili wa kijani ulivyopotea, badala yake maji yametanda kila mahali na kuonekana kama bahari.

Hapo awali maeneo hayo hayakuwa na hali hiyo, kwani rangi ya kijani ilitawala kutokana na kustawisha mazao kwa wingi, uwanda wa nyasi unaolisha idadi kubwa ya mifugo na pia watu walijenga nyumba zao kwa ajili ya kuishi.

Hata, hivyo kwa sasa vitu vyote vimeharibiwa na maisha ya watu yamerudi nyuma kiasi ambacho familia nyingi zimejikuta zikiishi kwa tabu kwa kukosa makazi.

Kibaya zaidi, mafuriko yamekuwa sawa na kaa la moto, yale matumaini ya kupata mavuno mazuri yamepotea kwani mazao yamezolewa, huku miundombinu barabara imeharibika vibaya.

Hali hiyo imemfanya Askofu wa Jimbo Katoliki la Lindi, Bruno Ngonyani, amepaza sauti akiomba taasisi binafsi, serikali na mashirika ya kimaifa kuangalia namna ya kusaidia watu ili kuwaepusha na makali ya mafuriko hayo.

Akinakiliwa kutoka mtandao wa Vatcan, Askofu Ngonyani, anasema Tanzania inashuhudia hali mbaya ya hewa kwa miezi kadhaa sasa. Anasema juhudi ya ziada zinatakiwa kufanywa ili kuhakikisha hakuna tatizo la kijamii litakalojitokeza.

Anasema kutokana na mvua kuendelea kunyesha kwa nguvu, kuna uwezekano wa kutokea upungufu wa chakula kwa waathirika.

Mbunge wa Rufiji, Mohammed Mchengerwa, amesema zaidi ya 500 zimekumbwa na maafa katika jimbo lake pekee na hekari zaidi ya 20,000 zilizolimwa mazao mbalimbali zimesombwa na maji.

Aidha inaonyesha wasiwasi wake kwamba inaweza kutokea athari njaa kutokana na mafuriko hayo.

Mchengerwa anaeleza kwamba kata karibia zote za jimbo hilo zimeguswa na maafa hayo,ikiwamo Muhoro,Chumbi ,Umwe na Ikwiriri.

Anasema katika kata ya Muhoro, zaidi ya 5,000 za mazao katika kata ya Muhoro zimeteketea na kata ya Chumbi hekari zaidi ya 8,000.

"Kimsingi mvua kwa hapa Rufiji si kubwa sana ,ila hili tatizo linasababishwa na maji kutoka Nyanda za Juu Kusini, mikoa ya Iringa na Morogoro yanatiririka kwenye mabonde na mabwawa,hofu kubwa inakuja kwamba Mtera nayo imeshafunguliwa, siku tatu hadi tano zijazo hali itakuwa mbaya zaidi ya hii":

"Maji yakiendelea kuwa kama hivi mashambani kuna wasiwasi wa kuwepo kwa njaa, maoni yangu ni kuangalia namna ya kuwasaidia wananchi hawa walioathirika," mbunge huyo alikaririwa wakati akikagua hali ya mafuriko katika kijiji cha Muhoro.

Hata hivyo, mbunge huyo anaeleza kwamba, kwa sasa anashirikiana na halmashuri kuangalia uwezekano wa kupata huduma muhimu wakati jitihada za kurekebisha athari zikifanyika.

Mkurugenzi wa Idara ya Uratibu wa Shughuli za Maafa Ofisi ya Waziri Mkuu, Kanali Jimmy Matamwe, anasema wakati serikali inaendelea kuratibu namna ya kukabiliana na athari hizo, kamati za usimamizi kuanzia ngazi za vijiji hadi wilaya zilizoundwa kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa maafa namba saba ya mwaka 2015 zinawajibika kutekeleza operesheni za dharura.

Mkuu wa Wilaya ya Rufiji, Juma Njwayo, anasema juhudi zinafanyika katika kurekebisha baadhi ya miundombinu iliyoharibika na kwamba serikali ipo macho kuwalinda wananchi wake.

"Wilaya tunaendelea na kukabiliana na maafa, kama tulivyoshauriwa kuhusu miundombinu, kwa kushirikiana na TANROADS tunaendelea kwa kasi kuchukua hatua za kurejesha miundombinu yote iliyo athirika " Amesisitiza Mhe. Njwayo.

Kwa mujibu wa Taarifa ya Mamlaka ya Hali hewa iliyotolewa mwezi Februari mwaka huu, imeeleza kuwa kutakuwa na mvua za juu ya wastani katika eneo kubwa la nchi, kati ya mwezi Machi hadi mwezi Mei, mwaka huu.

## HABARI KIMATAIFA

# Kenya yafikisha wagonjwa 246 corona

**NAIROBI,** Kenya

KENYA imetangaza kuwa na wagonjwa 246 wa corona, baada ya kuthibitisha watu 12 wapya wameambukizwa virusi vya Covid-9.

Taarifa ya Waziri wa Afya wa Kenya, Mutahi Kagwe, ilisema watu watano kati ya walioambukizwa ni wahudumu wa hoteli na kuongeza kuwa idadi hiyo ilifikiwa baada ya sampuli 400 kufanyiwa uchunguzi.

**Wizara ya Elimu itachukua hatua kuwalinda wanafunzi...**

Wakati idadi ya wagonjwa inaongezeka, Rais Uhuru Kenyatta, alitoa maagizo mapya ikiwamo kuitaka Wizara ya Afya na Huduma za Umma kuanzisha hazina ya kuwasaidia wafanyakazi wa afya wanaokabiliana na mlipuko wa virusi vya corona.

Pia, alisema Wizara ya Elimu itachukua hatua kuwalinda wanafunzi kutokana na athari mbaya za hatua zilizochukuliwa kukabiliana na Covid-19.

Mamlaka ya usambazaji wa tiba nchini Kenya, itaondoa masharti ya ununuzi wa vifaa vya kujilinda dhidi ya Covid-19, kwa takriban miezi mitatu ili kurahisisha kununua vifaa.

Kenyatta, alisema msaada utatolewa kwa usawa kupitia mfuko wa hali ya dharura wa kukabiliana na Covid-19.

Wakati huo huo, Kenya imepokea vifaa 40,000 vya kupimia, ikiwa ni katika harakati ya kuimarisha uwezo wa kupima watu haraka kwa lengo la kupima, kutengwa kwa walioathirika na kutibu.



Mwanamke mfanyabiashara wa matunda nchini Somalia, akimuuzia mteja wake kwa kufuata masharti ya afya ya kukaa mita mbili na mteja wake katika kujikinga na virusi vya Covid-19. **PICHA: REUTERS**

## Ujerumani yatangaza kudhibiti corona

**BERLIN,** Ujerumani

UJERUMANI imetangaza kudhibiti mlipuko wa kirusi cha corona baada ya miezi mitatu ya mapambano.

Waziri wa Afya, Jens Spahn, amewaambia waandishi wa habari jana mjini Berlin kwamba, ongezeko la wagonjwa wapya wa Covid-19 si la kutisha tena. Takwimu kutoka Taasisi ya Robert Koch, zinaonyesha kuwa, idadi ya maambukizi mapya imeshuka kwa 0.7 kutoka siku chache zilizopita.

Kansela Angela Merkel alisema wiki hii kwamba kile kinachoitwa kima cha uzalishaji ndicho kigezo kikuu kitakachoifanya serikali iamuwe kama italegeza uzuwiaji wa shughuli za kawaida kwa wananchi.

Kwa mujibu wa Spahn, tangu Aprili 12, idadi ya wanaopona maradhi hayo wamekuwa wengi kuliko wanaoambukizwa. Wataalamu wanasema hatua za upimaji wa awali na wa pamoja ziliisaidia sana Ujerumani kuzuia mlipuko huo kuwa mkubwa. **DW**

# WHO yaonya Afrika kuwa kitovu corona

**GENEVA,** Uswisi

SHIRIKA la Afya Duniani (WHO) limeonya Afrika huenda ikawa kitovu kipya cha mlipuko wa virusi vya corona.

Onyo hilo limetokana na kuongezeka kiasi kikubwa cha visa vya ugonjwa huo wiki iliyopita.

Takwimu iliyotolewa na Shirika hilo jana, inaonyesha katika kipindi hicho kumekuwa na zaidi ya visa 1,000 na maambukizi 18,000 barani Afrika. Hata hivyo viwango hivyo viko chini zaidi ya vile vinavyoonekana katika baadhi ya mataifa ya Ulaya na Marekani.

Shirika hilo limesema virusi hivyo vinaonekana kusambaa katika maeneo ya vijijini.

Pia limesema nchi nyingi za Afrika hazina mashine za kutosha za kuwasaidia wagonjwa kupumua ili kukabiliana na mlipuko huo.

Mkurugenzi wa Shirika hilo barani Afrika, Dk. Matchidizo Moeti, aliiambia BBC kwamba, shirika hilo limeshuhudia kuenea kwa virusi hivyo kutoka miji mikuu hadi vijijini katika mataifa ya Afrika Kusini, Nigeria, Ivory Coast , Cameroon na Ghana.

Alisema kwamba kwa sasa wanaangalia njia ya kuzuia badala ya kutibu virusi hivyo, kwa sababu mataifa hayo hayana uwezo wa kuwatibu wagonjwa wengi wa virusi vya corona.

"Tunataka kupunguza kiwango cha watu ambao wanafikia hatua ya kuhitaji mashine za kuwasaidia kupumua katika chumba cha wagonjwa mahututi, tunajua kwamba vifaa hivi ni vichache miongoni mwa mataifa mengi ya Afrika," alisema.

Alisema suala la mashine za kusaidia watu kupumua ni mojawapo ya changamoto kubwa ambazo mataifa hayo yanakabiliana nayo.

Mashine hizo zinasaidia mapafu kupumua na kutoa hewa chafu ya kaboni mwilini wakati mgonjwa anakuwa katika hali mbaya na hawezi kujisaidia kupumua.

## China yarekebisha idadi ya vifo

**BEIJING,** China

SIKU mbili baada ya Marekani kutangaza kuanza uchunguzi wa iwapo China ilificha ukweli kuhusu mlipuko wa kirusi cha corona, mji ambao kirusi hicho kilianzia, imerekebisha takwimu zake za idadi ya watu waliokufa kwa ugonjwa huo.

Mamlaka za mji wa Wuhan zimetangaza jana kwamba, kulikuwa na vifo 1,290 vya ziada, sawa na asilimia 50 ya idadi ya awali ya 3,869 vilivyokuwa vikifahamika.

Kulingana na taarifa hiyo, tatizo la vifo hivyo kutokufahamika ilitokana na ama kuripotiwa kimakosa au kupotoshwa moja kwa moja.

Kauli hiyo huenda ikaongeza wasiwasi miongoni mwa mataifa ya Magharibi dhidi ya uaminifu wa China kwenye janga hilo kilimwengu, ambalo hadi sasa limeshapoteza maisha ya watu 140,000 duniani kote.

Marekani, Uingereza na Ufaransa zina mashaka kwamba chanzo hasa cha kirusi cha corona ni maabara moja mjini Wuhan ambayo ilikuwa ikifanya utafiti kuhusu popo, na kwamba China haikulishughulikia tatizo hilo kwa umakini kwenye hatua za awali, wala haikusema kweli. **DW**

# HADITHI

# Mauaji Harusini- 8

ILISEMWA hapo zamani kuwa dunia inaharibiwa na vitu viwili tu. Mapenzi na mali. Vitu hivi vinaweza kumfanya binadamu aende popote. Afanye chochote kile ili awe navyo, wengine wanakwenda mbali zaidi mpaka ikiwezekana hata kutoa uhai wa wenzao.

Shani, binti wa kitajiri, anapitia kwenye mikasa mikubwa mizito ya kupotezwa kwa wazazi wake na kumsababishia ukiwa na mawazo tele. Wakati ikionekana binti huyo pekee kwa wazazi wake akielekea kurithi utajiri wa wazazi wake, kiu ya damu inaanza kuwaingia baadhi ya ndugu za wazazi wake ili apoteze maisha, wao waweze kumiliki mali hizo.

**Mtunzi anapatikana (0716 350534)**

**Na Adam Fungamwango**

NI kweli penzi halina macho, halina umri, rangi wala kabila. Penzi humea popote pale hata porini kama uyoga. Hata hivyo ni lazima kwanza kuna vitu vya kutazama kabla ya kuingia mzima mzima.

Tofauti isiyo ya kawaida ya umri ikizidi kwa wapendanao nalo ni tatizo. Lakini pia kuna umuhimu mkubwa ya kila mmoja kujua historia ya mwenzake wakati wa mapenzi, ili kama kuna shaka, basi kila mmoja anze uchunguzi, vinginevyo unaweza kujikuta umetumbukia kwenye penzi na ndugu yako.

Kimoyomoyo, Abesh alionekana kuwahusudu jamaa wale kutokana na jinsi wanavyoweza kutekeleza kazi na pia kujilinda.

Akiwa peke yake ndani alikuwa akijipongeza kwa kazi kubwa aliyoifanya ya kumuua Patiyo na mkewe Grace.

Patiyo, rafiki yake mkubwa kwenye masuala ya biashara kumgeuka na kumchukua mpenzi wake ambaye alitarajia kumuoa ni kitendo ambacho alikiona ni cha kumdhalilisha mtu kama yeye ambaye ni milionea na mwenye heshima kubwa nchini.

Alimkumbuka Grace, msichana aliyekuwa anampenda. Roho iliumuma kiasi kutokana na mapenzi aliyokuwa nayo juu yake, lakini hakuwa na la kufanya, kwani kitendo cha kumgeuka na kuanza uhusiano wa kimapenzi na rafiki yake, alikiona ni cha kisaliti, kumtia aibu na ukosefu wa adabu.

"Sikutaka kumuua, lakini umenilazimisha nifanye hivyo Grace. Nilikupenda sana, lakini hukuujali upendo wote juu yangu." Alijikuta akiongea peke yake.

Alikwenda kwenye friji na kutoa vichupa vitatu vya pombe kali, anavimimina kwenye glasi. Akachukua pia kidonge cha barafu na kutia kwenye glasi iliyokuwa na pombe. Akakaa kwenye kochi. Akainyanyua na kupiga mafunda kadhaa, miguu yake ikiwa mezani. Ilikuwa ni siku ya kufurahia ushindi wake, baada ya kukaa na sononeko kwa muda mrefu.

Yeye ni tajiri, hawezi kuchukuliwa demu na kuanza kulialia kama mtu ambaye hana mbele wala nyuma. Ni lazima afanye kitu. Alipize kisasi kama alivyofanya. Usingizi mzito ukampitia.

************************************

Asubuhi nchi ilianza na majonzi. Kwenye meza za magazeti kulijaa watu. Baadhi yao walikuwa wanatazama vichwa vya habari na wengine wakinunua. Gazeti la Nipashe liliandika vizuri zaidi habari za vifo vya maharusi wawili ambao walikufa masaa mawili tu baada ya kufunga ndoa. Kichwa cha habari kiliandikwa 'Mauaji Harusini.' Lilipambwa na picha kadhaa za maharusi walipokuwa hai wakitembea kwa madaha, wameshikana mkono, dakika chache kabla ya mdunguaji kuzima furaha yao.




**Na hata hivyo waliufanya kwa siri na mwenyewe Patiyo alidhani kitendo cha kufunga ndoa haraka haraka, kingeweza kumlainisha Abesh kusalimu amri moja kwa moja kwa sababu angekuwa mke wa mtu, lakini kumbe ndiyo alikuwa ameuwasha moto.**

Zilionekana picha ambazo wanafunga ndoa Kanisani, wanatoka nje. Wanaingia kwenye gari la kifahari, na hata zile ambazo wanashuka na kutembea kwa madaha, kabla mtu mmoja katili kudhulumu uhai wao.

Picha nyingine ulionekana umati wa watu nyumbani hapo baada ya tukio hilo.

Inawezekana ikawa ni moja kati ya ndoa zilizodumu kwa muda mfupi zaidi si nchini tu, bali hata dunia nzima na kilichowatenganisha si kuachana, ila ni kifo.

Na si kifo cha mtu mmoja tu bali wote wawili kwa wakati mmoja. "Masikini hawakuifurahia kabisa ndoa yao." Mama mmoja wa makamo alionekana kusikitika huku akiweka mikono kichwani kwenye meza moja ya magazeti maeneo ya Mwananyamala.

"Hawa wataenda peponi moja kwa moja, kwa sababu alifunga ndoa na wamekufa pamoja, tena wameuawa na watu wasiowatakia mema." Mama mwenzake alidakia.

Maeneo ya Kigamboni, tangu jioni ile hadi kesho yake hakukuwa na stori zingine. Ni ya mauaji ya maharusi.

Kikubwa zaidi ni mmoja wa maharusi hao ambaye ni bwana harusi kuwa ni mmoja wa wafanyabiashara mashuhuri nchini.

"Aliwadhulumu wenzake, nao wakaona sehemu ya kulipiza kisasi ni hii siku ya harusi, walimsubiri aoe ndiyo wamuue." Jamaa mmoja maeneo ya Tuangoma kule Kigamboni alikuwa akiwaambia wenzake mbele ya kibanda cha kuuzia magazeti walipokuwa wamejazana.

"Sasa kama walimuua kwa kulipiza kisasi, mbona wamemuua na mkewe?" Kijana mmoja aliyeonekana ni mdogo zaidi kuliko wenzake alimuuza?"

"Wewe unajua nini wewe, unawajua watu wakitaka kulipiza kisasi, wanaweza kufagia hadi watoto wako." Jamaa alitetea hoja yake.

"Jamani hata mimi mwenyewe namuunga mkono dogo huyu, inawezekana hiki kifo siyo kama jamaa aliwadhulumu wenzake, ila inawezekana mauaji haya wanaweza kuwa na uhusiano na hii hii ndoa yenyewe." Kijana mwingine aliyekuwa ametulia kwa muda mrefu alidakia.

"Ni kweli kabisa, kile kitendo cha kuuawa maharusi wote wawili, kinaonyesha kuwa aliyetekeleza mpango huo aliwakusudia wote wawili. Na wote wawili walimkera kwa alivyoona yeye." Mwingine alidakia.

"Sikilizeni nyinyi, haya mapenzi duniani yana matatizo sana, inawezekana demu alimkataa mshikaji akaamua kuolewa na tajiri, kwa hasira zake kaamua kufanya hivyo." Kijana mmoja aliyekuwa akivuta sigara alidakia.

Hakuna aliyeongea kitu baada ya hapo, bali karibuni wote walimuangalia kwa makini. Huenda kwenye mioyo yao waliona yuko karibuni na ukweli. Hata hivyo wote walikuwa wanadhania tu, hakuna aliyekuwa na uhakika sababu hasa ni nini.

************************************

Mazishi wa maharusi hao walifanyika pamoja. Walizikwa kwenye makaburi ya Kinondoni jijini Dar es Salaam na kuhudhuriwa na maelfu ya watu. Achilia mbali umaarufu wa mfanyabiashara mkubwa Patiyo Alphonce, lakini pia aina ya kifo chenyewe jinsi kilivyowagusa watu wengi na kuchukua nafasi kubwa ya habari kwenye mitandao ya kijamii, magazeti, mitaani na sehemu mbalimbali za kijamii.

Shani, binti pekee wa Patiyo akiwa anasaidiwa na rafiki zake. Akiwa na miaka 23 tu, bado alikuwa msichana mbichi ambaye alitakiwa awe anaendelea kudeka kwa baba na mama yake, lakini haikuwa hivyo.

Mama yake alifariki miaka 10 iliyopita akiwa na miaka 13 tu, akiwa kwenye harakati za kujifungua kichanga ambacho kingekuwa ni mtoto wa pili, lakini pia ni mdogo wa Shani. Mungu alimchukua mama Shani na kichanga hiyo. Akabaki na baba yake ambaye alimlea na kumsomesha kwa mapenzi makubwa.

Patiyo hakutaka kuoa tena kwa kuhofia mtoto wake kupata tabu, hivyo aliamua kukaa bachela kwa miaka yote hiyo.

Hata hivyo alimpata mwanamke aitwaye Grace Maumba, aliyeondokea kumchengua vilivyo na kuamua sasa kuoa.

Kwanza aliona tayari binti yake ameshakuwa mkubwa na hata kama akioa, kwa umri wa binti yake hawezi kuteswa, lakini pia alitaka azae watoto wengine ambao wako ndani ya ndoa. Pia alipata ushauri na ruhusa kutoka kwa binti yake kipenzi, Shani.

Suala la Grace kuwa alikuwa ni mpenzi wa Abesh alilifahamu fika, lakini pia walipokorofishana na kila mmoja kuchukua hamsini zake alilifahamu pia.

Wakati Abesh akidhani kuwa Grace ameamua kumpiga chini kwa sababu ya Patiyo, lakini ukweli ni kwamba Patiyo alianza mahusiano na Grace, miezi sita baada ya kuachana na Abesh.

Na hata hivyo waliufanya kwa siri na mwenyewe Patiyo alidhani kitendo cha kufunga ndoa haraka haraka, kingeweza kumlainisha Abesh kusalimu amri moja kwa moja kwa sababu angekuwa mke wa mtu, lakini kumbe ndiyo alikuwa ameuwasha moto.

Shani, ambaye pamoja na umri mdogo akiwa ni msomi, kwa sababu alipelekwa shule za gharama kubwa, tena akiwa na umri mdogo, lakini tayari mazingira yalimfanya akue kabla ya umri wake.

Akiwa ni mtoto pekee alijua kuwa anakabiliwa jukumu la kurithi utajiri wa baba yake na kuuendesha ili uzidi kuendelea badala ya kushusha chini au kuua kabisa.

Kwa bahati nzuri baba yake hakumtenga, bali alijua mali zote za baba yake na pia jinsi ya kuziendesha kwa sababu Patiyo hakutaka binti yake pakee apoteze muda mwingi kusomea vitu vingine, badala yake alimpeleka nje nchi kusomea biashara na utawala.

Hata hivyo pale msibani akili yake ilikuwa kama nusu mfu. Pamoja na yote yale, lakini hakutegemea baba yake kufa mapema kiasi kile, tena kwa aina ile ya kifo.

ITAENDELEA JUMAMOSI

# TMA yafafanua kuhusu mwanga ulioonekana

**Na Romana Mallya**

MAMLAKA ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA), imetoa ufafanuzi kuhusu tukio la kuonekana mwanga wa rangi ya chungwa angani juzi na kusababisha taharuki kwa wananchi.

Mkurugenzi Mkuu wa TMA, Dk. Agnes Kijazi, akizungumza na Nipashe, alisema kilichoonekana siku hiyo kilikuwa ni mwanga wa upinde wa mvua (rainbow) kujitokeza katikati ya wingu la mvua.

Juzi, majira ya saa moja kasoro usiku katika maeneo mbalimbali likiwamo jiji la Dar es Salaam kulitokea mwanga huo na kuzua taharuki, huku wengine wakihusisha tukio hilo na masuala ya kiimani.

"Jana (juzi) kulikuwa na mawingu na wakati huo huo upinde wa mvua ulikuwa umejitokeza na jua lilikuwa halijazama, kwa hiyo, mionzi ya jua ilivyoingia kwenye mawingu badala ya rangi za upinde wa mvua kuonekana, ukatokea mwanga," Dk. Kijazi alifafanua.

Kwa mujibu wa taarifa ya mamlaka hiyo, mwonekano huo wa anga wenye rangi ya chungwa au nyekundu ni hali ya kawaida ambayo hutoka wakati jua linapozama au kuchomoza katika mazingira yenye hewa kama mawingu.

"Hali hiyo husababisha kutawanywa kwa miale ya mwanga wa jua, kutokana na ukubwa wa matone ya maji katika wingu na chembechembe za vumbi katika anga.

"Sehemu ya miale ya jua inayotawanywa zaidi katika mazingira hayo ni mawimbi ya miale ya jua inayohusiana na rangi nyekundu au chungwa hivyo kufanya anga kuonekana katika rangi hizo."

Alisema hali hiyo haina tofauti na upinde wa mvua unavyojitokeza angani, isipokuwa upinde wa mvua unakuwa na rangi zote saba za spectrum ya mwanga.

"Mabadiliko hayo ya hali ya anga hayana madhara yoyote, alisema.

# Bosi TAA aachiwa huru kesi ya usafirishaji nyara

**Na Hellen Mwango**

WATU wanne akiwamo Meneja wa Usalama wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege (TAA), Clement Jingu, wameachiwa huru na Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, baada ya Jamhuri kushindwa kuthibitisha mashtaka ya kushiriki kusafirisha nyara za Serikali na matumizi mabaya ya madaraka.

Mbali na Jingu, washtakiwa wengine ni maofisa usalama, Emmanuel Nyambele, Salum Seifu na Akbadru Habibu.

Hukumu hiyo ilisomwa jana na Hakimu Mkazi Mkuu, Huruma Shaidi baada ya kusikiliza mashahidi wa pande zote mbili bila kuacha shaka mahakama yake iliwaona hawana hatia.

Alisema baada ya kupitia ushahidi ni wazi kwamba umejikita kwenye ushahidi wa kielekitroniki, pia maelezo ya washtakiwa waliyotoa Polisi.

"Upande wa Jamhuri ulishindwa kujenga msingi wa kesi dhidi ya washtakiwa na kwamba umejielekeza katika ushahidi mwingine wa mawasiliano, swali la kujiuliza ni je, kesi ilijengwa katika misingi ya kisheria, sheria inaelekea kesi lazima ithibitishwe bila kuacha shaka," alisema Hakimu wakati akiichambua hukumu hiyo.

Alisema mshtakiwa wa kwanza Julai 5, 2015 hakuwapo kazini, lakini hakutakiwa yeye kuthibitisha kwa kuwa hilo ni jukumu la upande wa Jamhuri kuithibitishia mahakama.

"Katika ushahidi wa elektroniki tumeona kamera ya CCTV ilionyesha mabegi yakipita lakini haikuonesha mabegi hayo yalikuwa yana kitu gani ndani" alisema Hakimu Shaidi.

Alisema maelezo ya onyo ya washtakiwa yalipingwa wakati kesi inasikilizwa, na kuwa maelezo hayo yalichukuliwa chini ya kifungu cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai namba 58.

Kifungu hicho kinaelekeza maelezo yaandikwe na mtuhumiwa mwenyewe, lakini katika kesi hiyo maelezo yaliandikwa na Polisi.

"Maelezo haya yana shida, ushahidi wake hauna nguvu katika shauri hili," alieleza Hakimu Shaidi na kuongeza:

"Ushahidi wa mawasiliano ni wa mazingira, lazima uwapo ushahidi mwingine wa kuunga mkono, ushahidi huu hauwezi kuchukuliwa kuthibitisha kosa.

Kwa mantiki hiyo, kosa la kula njama halijathibitika kwani hakuna mahali katika ushahidi ukionyesha kwamba washtakiwa waliwahi kukaa na kufanya vikao."

Alisema kwa mshtakiwa wa pili na watatu na wanne pia kosa hilo halijathibitika.

Alisema Serikali iliomba kielelezo cha nyara hizo Uswisi wakakataa kuleta, hivyo hali hiyo inaleta utata kisheria.

Alisema upande wa Jamhuri ulipeleka 'sample' kama nyara zilizosafirishwa, jambo ambalo halikubaliki, badala yake walipaswa kuwasilisha mahakamani kielelezo cha nyara zilizokamatwa.

Alisema Serikali ya Uswisi haikutenda sawa, na ndio wamesababisha haya.

"Makosa hayajathibitishwa kama inavyotakiwa, washtakiwa nawaachia huru, ambaye hajaridhika anaweza kukata rufani," alisema Hakimu.

Washtakiwa walikuwa wakikabiliwa na mashtaka manne, likiwamo la kuchora michoro ya kihalifu ya kusafirisha nyara za Serikali zenye thamani ya Sh. milioni 267.4 na matumizi mabaya ya madaraka.

Inadaiwa Julai 5, 2015, katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Mwalimu Nyerere (JNIA) washtakiwa hao walikula njama ya kusafirisha nyara za Serikali.

Ilidaiwa kuwa kati ya Julai 2 na 6, 2015 katika uwanja huo, kwa makusudi waliendeleza michoro ya kihalifu kwa kuruhusu usafirishwaji wa kilo 150 za meno ya tembo, meno ya simba 21 na kucha za simba 35.

Inadaiwa Julai 5, 2015, washtakiwa hao walifanya hivyo bila ya kuwa na kibali cha usafirishaji kutoka kwa mkurugenzi wa wanyamapori.

Washtakiwa hao pia walidaiwa kuwa kati ya Julai 2 na 5, mwaka huo wakiwa waajiriwa wa TAA, walitumia vibaya madaraka yao kwa kusaidia kusafirisha nyara hizo wakati ni ukiukwaji wa Kifungu cha 82 (1) na 84(1) cha Sheria ya Wanyama Pori Sura namba 5 ya mwaka 2009.



Mjumbe wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), Jaji mstaafu Stella Longway (kulia), akikagua shughuli ya uboreshaji wa daftari la kudumu la wapigakura katika Kata Longuo 'B', Manispaa ya Moshi, mkoani Kilimanjaro jana. **PICHA: ALLAN LSACK**

# Wakazi 45,076 wapima VVU kwa hiyari Namtumbo

**Na Gideon Mwakanosya,** NAMTUMBO

JUMLA ya watu 45,076 wamejitokeza kupima kwa hiari virusi vya Ukimwi (VVU) katika Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo mkoani Ruvuma katika kipindi cha mwaka 2019.

Hayo yamesemwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Evance Nachimbinya, alipokuwa anatoa taarifa ya utekelezaji wa shughuli za kudhibiti maambukizi ya VVU kwa Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Christina Mndeme, mjini Namtumbo.

Nachimbinya alisema kati ya waliopimwa watu 587 waligundulika kuwa na maambukizi, na kwamba kiwango cha maambukizi katika Halmashauri hiyo kimepungua kutoka asilimia mbili mwaka 2018 hadi asilimia moja mwaka 2019.

Hata hivyo, alisema katika kipindi hicho wanaume ndiyo wamejitokeza kwa wingi kupima kwa hiari ambapo jumla ya 30,303 walipima kwa hiari ukilinganisha na wanawake waliokuwa 14,773.

"Wote waliobainika kuwa na maambukizi walisajiliwa katika vituo vya tiba na matunzo kwa ajili ya usimamizi wa afya zao ili kuimarisha afya zao na wapate nguvu za kuendelea kulitumikia Taifa," alisisitiza Nachimbinya.

Ameyataja mafanikio ambayo Halmashauri hiyo imeyapata katika kukabiliana na Ukimwi kuwa ni kutoa huduma ya tiba na matunzo kwa waishio na VVU, upimaji kufanyika katika ngazi zote za kutolea huduma za afya ili kufikia malengo ya 95.

Alizitaja changamoto zilizojitokeza katika kipindi hicho ni kupungua kwa mchango wa wadau kutokana na kupungua kwa bajeti ya mfadhili mkuu kwa serikali na changamoto ya usafiri katika vituo husika kutokana na Halmashauri kuwa na upungufu mkubwa wa magari.

Mkuu wa Mkoa, Mndeme aliwapongeza wanaume kwa kujitokeza kwa wingi kupima afya zao.

Mndeme alosema kitendo hicho kitaiwezesha serikali kufikia malengo yaliyopangwa ya kuwa na jamii salama, kutokana na maambukizi mapya ya VVU ifikapo mwaka 2030 kumaliza kabisa maambukizi.

# MATTHAUS: UPAMECANO USIONDOKE LEIPZIG



**MUNICH,** Ujerumani

DAYOT Upamecano, anatakiwa kufikiria mara mbili kuhusu mpango wake wa kuondoka RB Leipzig na kujiunga na Bayern Munich au klabu nyingine kubwa ya Ulaya mwishoni mwa msimu huu, kwa mujibu wa Lothar Matthaus.

Miamba hao wa Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga Bayern, wametajwa kujiunga na Real Madrid na klabu kadhaa za Ulaya katika mbio za kuwania saini ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21.

Mchezaji huyo wa timu ya taifa ya Ufaransa chini ya umri wa miaka 21, ameichezea mechi 76 Leipzig tangu alipojiunga kutoka Salzburg mwaka 2017, na kuvutia jicho la klabu kadhaa.

Klabu zinazomwania mlinzi huyo wa kati zinaweza kuongezeka, lakini gwiji wa Bayern, Matthaus amebainisha kwamba kuondoka pale kwenye uwanja wa Red Bull Arena baadaye mwaka huu hautakuwa uamuzi sahihi.

"Namwona kwamba ana uwezo wa kucheza kwenye klabu yoyote kubwa na kupata uzoefu zaidi," amesema Matthaus akiiambia Sky Sport Germany.

"Kama ataondoka, anahitaji kuhakikisha kwamba kocha wake mpya au klabu atakayokwenda inampa ujasiri wa kucheza mara kwa mara - kama anavyofanya pale Leipzig.

# Maguire: Najadiliana na klabu kuhusu mshahara

**MANCHESTER,** England

NAHODHA wa Manchester United, Harry Maguire, amebainisha kwamba, kwa wiki sasa amekuwa akijadiliana na klabu kuhusu kukatwa mishahara wakati huu wa mlipuko wa virusi vya corona.

Maguire amesema kila klabu zitakumbana na matatizo ya kifedha kutokana na corona, lakini United haitatumia sera ya serikali ya kupeleka watu likizo na malengo yao ni kuwalinda wafanyakazi 900 ambao wanafanya kazi muda wote.

Maguire ameiambia Sky Sports: "Nafikiri kwanza kila klabu mfumo wake utakuwa tofauti.

"Nimekuwa nikijadiliana na klabu kwa wiki namna gani tutakwenda mbele bila kuathiri ajira ya mfanyakazi hata mmoja.

"Nina uhakika kila wiki watachambua, kuangalia wapi tulipo na kama tunaweza kufanya kitu chochote kuhusiana na hali hiyo ya kukata mishahara.

"Kila klabu itakuwa tofauti, tofauti na mfumo na nina uhakika kila nahodha atazungumza kwa niaba ya klabu."

Wakati Ligi Kuu England ikisimama, United wao wapo nafasi ya tano kwenye msimamo wa ligi hiyo, huku pia wakiwa bado kwenye mashindano ya Kombe la FA na lile la Europa.






# Mascherano ana matumaini Neymar kurudi Barcelona

**BARCELONA,** Hispania

NYOTA wa zamani wa Barcelona, Javier Mascherano, ana matumaini mkali wa Paris Saint-Germain, Neymar, atarudi kwa mabingwa wa Ligi Kuu Hispania, LaLiga, kucheza pamoja na Lionel Messi na Luis Suarez.

Neymar aliondoka Barca kwenda PSG kwa ada iliyoweka rekodi ya euro milioni 222 mwaka 2017, lakini nyota huyo wa kimataifa wa Brazil mara kwa mara amekuwa akihusishwa na mpango wa kurudi pale Camp Nou. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28 alikaa miaka minne pale Barca, ambako alishinda mataji mawili ya LaLiga na moja la Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Mascherano alikuwa mchezaji mwenzake na Neymar wakati Barca walipotwaa taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu wa 2014-15 wakishinda 3-1 dhidi ya Juventus mjini Berlin na nahodha huyo wa zamani wa Argentina anatoa taswira ya usiku ule pale kwenye dimba la Olympiastadion.

"Siku chake tena nimeangalia ile fainali ya mjini Berlin na namna gani washambuliaji watatu pale mbele walivyokuwa wakivutia, Neymar, Suarez na Messi," amesema Mascherano akiiambia RAC1.

## HABARI MICHEZO

# Mourinho alikubali kuifundisha Liverpool

**LONDON,** England

JOSE Mourinho alikubali kujiunga na Liverpool mwaka 2004 ili kuchukua mikoba ya Gerard Houllier, lakini mmiliki wa Chelsea, Roman Abramovich alimfuata kwa dau kubwa na la juu lililobadilisha uamuzi wake.

Kitabu kipya cha Mreno huyo, "Mourinho: Nyuma ya Mtu maalumu, kuanzia mwanzo hadi ufalme wake," imebainika.

Kitabu hiko kikiwa kimeandishwa na Mwandishi wa Habari Mfaransa, Nicolas Vilas, kimeeleza namna Mourinho alivyokaribia kutua Liverpool miaka 16 iliyopita.

Aprili mwaka 2004, akiwa na kikosi cha Porto alikabiliwa na mechi ngumu ya hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Lyon, mshauri wa Mourinho, Jorge Baidek, alifanya kikao maalumu na kocha huyo kuelekea mchezo huo.

"Mourinho alitakiwa kujiunga na Liverpool. Rick Parry [halafu Mkurugenzi Mtendaji] alikuwa ndio aliyesimamia uhamisho huo na walifikia makubaliano. Walitueleza tusubiri kwa siku 15 wakati Houllier akiwa bado anaongoza Redsr," alisema Baidek.

Mourinho alijiandaa kutua Anfield, wakala huyo Mfaransa Bruno Satin naye alijumuishwa katika mazungumzo hayo.

Hata hivyo, wakala Jorge Mendes, alikuja baadaye akiwa na ofa nono akiwawakilisha Chelsea, kitabu hicho kiliendelea kuandika. Ingawa huko nyuma hakuwahi kufanya kazi na Mourinho, ofa iliyowekwa mezani ilikuwa kubwa kuliko iliyoletwa na klabu hiyo ya Merseyside.



# RAKITIC HAJAOMBA KUONDOKA – KOCHA



**BARCELONA,** Hispania

KOCHA Quique Setien, amesisitiza Ivan Rakitic, hajaomba kuondoka Barcelona, huku akisema ni mapema mno kujadili kuhusu majaliwa ya Philippe Coutinho.

Mkataba wake ukiwa unamalizika mwaka 2021, Rakitic hivi karibuni aliishutumu klabu hiyo ya LaLiga namna ilivyomchukulia na kiungo huyo wa kimataifa wa Croatia anaonekana kukaribia kuondoka.

Lakini Setien amebainisha kwamba, alikuwa hajui kama mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32 alikuwa na mpango wa kuondoka na amesema ameridhishwa na kiwango cha Rakitic msimu huu.

"Sina taarifa kama Rakitic anataka kuondoka na hajawasilisha ombi hilo kwangu. Na kwa upande wangu amecheza kwa muda mwingi na kwa kiwango kizuri na anaendelea kufanya hivyo," amesema akiliambia gazeti la El Larguero, juzi Alhamisi.

"Nina furaha na kiwango chake na sina cha kusema. Tunatakiwa kusubiri na kuona nini kitatokea na kama anataka kuondoka au la. Na kama natakiwa kusema hivyo, muda utakuja."

Mchezaji mwingine ambaye amekuwa akihusishwa na mpango wa kuondoka moja kwa moja hapo Barcelona ni Coutinho, ambaye alikuwa akicheza kwa mkopo pale Bayern Munich msimu huu.

Kiungo huyo mshambuliaji alikuwa na msimu mgumu kwake pale Barca, lakini Setien amesema alikuwa shabiki wa mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil.

"Ni mchezaji mkubwa na mara zote nilikuwa napenda kumwangalia anavyocheza, lakini ni mapema mno kuzungumzia majaliwa yake," alisema.

# Serie A kuanza mazoezi Mei

**ROME,** Italia

WAZIRI wa michezo wa Italia, Vincenzo Spadafora, ana matumaini kwamba ifikapo Mei 4, mwaka huu itathibitishwa rasmi kuanza kwa mazoezi ya Ligi Kuu Italia maarufu Serie A.

Serie A ilisimamishwa Machi, mwaka huu baada ya baadhi ya mechi kuchezwa kwenye viwanja visivyo na mashabiki, kutokana na mlipuko wa virusi vya corona, ambavyo vimegharimu maisha ya zaidi ya watu 145,500 duniani kote hadi jana.

Shirikisho la Soka la Italia, FIGC, tayari lilibainisha kwamba, ligi hiyo haitaanza tena hadi hali ya kiafya na usalama itakapotengamaa.

Serikai ya Italia imeongeza muda wa kuendelea kukaa ndani hadi Mei 3, ingawa tayari baadhi ya klabu zimeripotiwa kutaka kuanza mazoezi kabla ya siku hiyo ili kuwa na mwezi mmoja wa kumaliza msimu wa 2019-20.

Akizungumzia uwezekano wa kuanza kwa mazoezi mwezi ujao, Spadafora amewaambia waandishi wa habari: "Wiki chache zijazo ndio tutaelewa hali halisi ya afya na usalama.

"Tutaangalia kama timu zitaweza kuanza kurudi kwenye mazoezi ya kuendelea na Ligi au la, lakini hadi Mei 4, mwaka huu ndio itaweza kuthibitika rasmi.

"Tuna matumaini kila kitu kitakuwa sawa Mei 4, na hapo tutaangalia kama mazoezi yataanza kwenye viwanja bila mashabiki."

Wakati ligi hiyo inasimama, Juventus wanaongoza msimamo wa ligi hiyo kwa tofauti ya pointi moja dhidi ya Lazio iliyopo nafasi ya pili baada ya mechi 26.

Italia hadi jana ilirekodi jumla ya vifo vya watu 22,100 zilivyotokana na maambukizi ya virusi vya corona.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# BENZEMA ASHIKILIA USAJILI WA HAALAND

**Ni kutokana na Mfaransa huyo kuwa nguzo muhimu kwa Madrid tangu Ronaldo alipoondoka...**

**MADRID,** Hispania

MPANGO wowote wa Real Madrid kumsajili Erling Braut Haaland, utategemea na kiwango cha fowadi wao, Karim Benzema, ambaye amekuwa chaguo lao la kwanza klabuni hapo, kwa mujibu wa ripoti kutoka nchini Hispania.

**Nyota huyo wa Dortmund, Haaland, amekuwa na kiwango cha kuvutia na klabu kadhaa kubwa zimekuwa zikimtolea macho, huku akiwa amefunga mabao 40 msimu huu.**

Klabu kubwa duniani sasa zinamwangalia kwa karibu zaidi mshambuliaji huyo wa kimataifa wa Norway na Madrid nayo inamwania, lakini uhamisho wa kutua kwa klabu hiyo yenye maskani yake mji mkuu wa Hispania, yatategemea zaidi na kiwango cha Benzema, gazeti la AS limedai.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa anapanga kubakia na Los Blancos hao hadi mwishoni mwa mkataba wake mwaka 2022, na amekuwa kwenye kiwango bora tangu kuondoka kwa Cristiano Ronaldo klabuni hapo, na itakuwa ngumu kwa kocha, Zinedine Zidane kumwondoa kwenye kikosi cha kwanza kwa sasa, ripoti inasema.

Ripoti hiyo imebainisha kwamba, Benzema amekuwa na mchango mkubwa mno kwa kikosi hicho tangu kuondoka kwa Ronaldo raia wa Ureno aliyetimkia Juventus mwaka 2018.

Amefunga asilimia 24 ya mabao msimu huu, huku msimu uliopita akifunga kwa asilimia 30.

Kumsajili Haaland "litakuwa tatizo kwa Zidane", limeandika gazeti la AS, kwani atatakiwa kwanza kuzoea mfumo ambao tayari Benzema ameshauzoea na kujijengea jina kubwa.

Benzema ni mmoja wa wachezaji wa muda mrefu zaidi pale Madrid, pamoja na Sergio Ramos na Marcelo, wakiwa wamekaa na klabu hiyo kwa miaka 11 sasa.

Tangu alivyojiunga Real akitokea Lyon mwaka 2009, amefunga mabao 241 na ameshinda kila kitu, huku mara mbili na Ligi ya Mabingwa Ulaya mara nne.

## ZISIKUPITE

### BELLINGHAM AKARIBIA UNITED

MANCHESTER United inaongoza katika mbio za kuwania saini ya kiungo wa Birmingham ambaye ni raia wa England, Jude Bellingham (16). Thamani ya kinda huyo imetajwa kuwa ni pauni milioni 35, huku Chelsea na Borussia Dortmund pia zinatajwa kumwania Bellingham. ***(Sun)***

### RODRIGUEZ SAFARI YAIVA

WAKALA wa mshambuliaji wa Real Madrid na Timu ya Taifa ya Colombia, James Rodriguez (28), amefanya mawasiliano na Manchester United kujadili uhusiano wa kujiunga na klabu hiyo katika majira ya joto. ***(Sport via Metro)***

### GREALISH ATAJWA EVERTON

EVERTON inajiandaa kumsajili kiungo wa Aston Villa, Jack Grealish (24), lakini itafanya hivyo kama itahakikisha kuwanasa wachezaji wengine ambao inawahitaji. Kwa sasa The Blues pia wameonyesha nia ya kumsajili mshambuliaji wa Gremio na Timu ya Taifa ya Brazil, Everton Soares, 24. ***(Sky Sports)***

### MAGALHAES AGOMBEWA

MABOSI wa Everton wameanza mazungumzo ya kumsajili beki wa Lille, Mbrazili Gabriel Magalhaes. Chelsea na Arsenal pia zinamwania nyota huyo mwenye umri wa miaka 22. ***(Guardian)***

### EVERTON YAMFUATA IMMOBILE

KLABU ya Everton inataka kumsajili straika wa Lazio na Timu ya Taifa ya Italia, Ciro Immobile (30), na wako tayari kumtoa nyota wake Moise Kean (20), kama sehemu ya mchakato wa usajili huo. ***(Teamtalk)***

### BROZOVIC ANUKIA LIVERPOOL

LIVERPOOL imeanza mazungumzo na kiungo wa Inter Milan na Timu ya Taifa ya Croatia Marcelo Brozovic (27), kutua klabuni kwake. ***(Libero via Express)***

### MADRID KUMBAKISHA JOVIC

REAL Madrid inajiandaa kumbakisha klabuni hapo straika anayewindwa na Arsenal, Luka Jovic. Nyota huyo raia wa Serbia mwenye umri wa miaka 22, amecheza kwa dakika 90 zote katika mechi moja msimu huu akiwa na vigogo hao wa Hispania. ***(Sport via Sun)***

### ROBERTS ANUKIA CELTIC

CELTIC imeanza mazungumzo na Manchester City kuhusiana na kumrejesha klabuni kwake winga, Patrick Roberts kwa dau la pauni milioni tatu. Nyota huyo kwa sasa yuko kwa mkopo Middlesbrough, na huko nyuma aliwahi kuitumia Celtic kwa mkopo wa misimu miwili. ***(Teamtalk)***

### COUTINHO ATAKIWA BARCA

BARCELONA bado inamhitaji katika kikosi chake kiungo Philippe Coutinho, kwa ajili ya msimu ujao, Kocha Quique Setien, amesema. Mbrazil huyo mwenye umri wa miaka 27 yuko kwa mkopo Bayern Munich, na anahusishwa na Chelsea na Tottenham. ***(Evening Standard)***

### CHIESA AWEKWA SOKONI

WINGA Mtaliano Federico Chiesa ataondoka Fiorentina kwa dau sahihi, rais wa klabu hiyo ameeleza. Manchester United, Juventus na Inter Milan zimeonyesha nia ya kumwania nyota huyo mwenye umri wa miaka 22. ***(Sky Italia - in Italian)***

## HABARI MICHEZO

# Ihefu yatambia mastraika wake

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Ihefu FC ya jijini Mbeya, ambayo inashiriki Ligi Daraja la Kwanza umesema wanajivunia ubora wa safu yao ya washambuliaji na wanaamini ndiyo inayowabeba kuelekea Ligi Kuu Bara msimu ujao.

Katibu Mkuu wa Ihefu, Fred Chalamila, alisema uimara wa safu ya ushambuliaji waliyokuwa nayo ndio silaha pekee iliyowapa matokeo mazuri katika mechi mbalimbali walizocheza msimu huu.

Chalamila alisema kuwa, wanawaandaa washambuliaji hao kuongeza umakini ili wapate matokeo chanya katika mechi nne zilizobakia za kumalizia msimu.

"Hofu yetu ni washambuliaji kuongeza umakini zaidi, tumeliomba benchi la ufundi kwa kipindi hiki cha mapumziko ya corona kuwapatia programu maalum ili kuimarisha viwango vyao kwa sababu tunahitaji kumalizia vita," alisema Chalamila.

Alisema wamebakiza mechi mbili nyumbani na mbili za ugenini, hivyo wanajiimarisha kusaka matokeo mazuri.

Ihefu yenye pointi 39 sawa na wapinzani wao Dodoma FC wako katika nafasi ya pili ya msimamo wa Kundi A wakiwa na mabao 24 wakati vinara wana magoli 28.



# Mawenzi bado yawekwa sokoni

**Na Frank Kaundula,** MOROGORO

CHAMA Cha Soka Mkoa wa Morogoro (MRFA), kimeutaka uongozi wa Mawenzi Market kufuata taratibu katika mchakato wa kuiuza timu hiyo ili kuepusha kutokea kwa migogoro ndani ya klabu hiyo.

Ushauri huo ulisemwa jana na Katibu wa MRFA, Hamis Semka, baada ya ofisi yake kupokea barua kutoka kwa uongozi wa Mawenzi Market ikieleza nia ya kuiuza timu hiyo baada ya kushindwa kuiendesha kikamilifu.

Semka alisema viongozi wanatakiwa kuwashirikisha wanachama wao hatua zote za mipango ya kuiuza klabu yao na kwa kufanya hivyo hawatavunja kanuni.

Naye Mwenyekiti wa timu hiyo, Awadhi Mlongachaka alisema changamoto ya ukata na madeni mbalimbali yanayowakabili ndiyo imesababisha kufikia uamuzi huo.

Mlongachaka alisema endapo watakosa mnunuzi, timu hiyo itakuwa katika hatari ya kushuka daraja kwa sababu hawana fedha ya kusafirisha kikosi kwenda kwenye mechi za ugenini.

# NAMUNGO KUSAJILI NYOTA WACHACHE MSIMU MPYA

**Na Saada Akida**

ILI kuwa na kikosi imara kitakachokabiliana na ushindani, Kocha Mkuu wa Namungo FC, Thiery Hitimana, amesema atasajili wachezaji wapya wachache ili kuimarisha nafasi ambazo zitakuwa na upungufu.

**Tayari wachezaji wawili wa Namungo, kiungo Luka Kikoti anahusishwa kuwindwa na Simba wakati mshambuliaji, Reliants Lusajo anatakiwa Yanga.**

Akizungumza na gazeti hili jana, Hitimana alisema mabadiliko atakayofanya yatagusa nafasi chache na anaamini uamuzi huo utalenga kuimarisha timu hiyo ili kuendeleza ushindani katika msimu mpya.

Hitimana alisema tayari ameshaanza kusaka wachezaji katika nafasi ya kiungo na washambuliaji, ili kuziba pengo litakaloachwa na nyota wake wanaotakiwa na vigogo wa Ligi Kuu Bara, Simba na Yanga.

"Tayari kuna taarifa baadhi ya nyota wangu wameanza kutajwa na timu nyingine, sasa huu ni muda sahihi wa kuangalia mbadala wao endapo watafanya uamuzi wa kuondoka, hii itasaidia kutotetereka kwa timu yangu," alisema Hitimana.

Aliongeza anaamini wachezaji atakaowasajili watafanya vizuri kutokana na uwezo wake wa kukuza vipaji alionao.

"Mipango yangu ni kuona msimu ujao tunaendelea kufanya vizuri, sitafanya mabadiliko makubwa, ila nitalazimika kusajili wachezaji wapya katika nafasi ambazo nyota wake wataondoka," alisema Hitimana.

Kocha huyo ambaye mkataba wake unatarajiwa kumalizika mwishoni mwa msimu huu, aliweka wazi mipango yake ni kuhakikisha Namungo inaendelea kutoa ushindani katika kila mechi wanayocheza.

**PAMBANA...**



Vijana wakicheza mchezo wa pool katika eneo la Kitunda, Kivule jijini Dar es Salaam jana. **PICHA : JUMANNE JUMA**




# *Ngasa aendelea kujiimarisha Pwani*

**Na Mwandishi Wetu**

KIUNGO wa Yanga, Mrisho Ngasa, amesema anautumia vema muda wa mapumziko kwa kufanya mazoezi ili Ligi Kuu Tanzania Bara itakavyorejea, awe kwenye ubora wake uliozoeleka.

Akizungumza na gazeti hili jana, Ngasa alisema anatekeleza programu zote alizopewa na kocha wake kwa sababu anafahamu ligi itakaporejea, mechi zitakuwa na ushindani zaidi kutokana na kila timu kujipanga kutimiza malengo yake.

Ngasa alisema mara zote mechi za lala salama huwa na changamoto mbalimbali na yeye kama mchezaji mzoefu, anajiandaa kuisaidia timu kupata matokeo mazuri katika mechi zote zilizosalia.

"Kwa sasa niko Bagamoyo, nimetafuta sehemu nzuri yenye utulivu kwa ajili ya kufanya mazoezi, nafanya hivi ili kulinda kipaji changu, nikimaliza programu ya kujifua, ninapata pia muda wa kupumzika," alisema Ngasa.

Aliwakumbusha wachezaji wote kuongeza bidii katika mazoezi yao kwa sababu kila mmoja atatakiwa kutekeleza vema majukumu yake pale ligi itakaporejea tena.

"Namshangaa Kaseke (Deus), bado yupo Mbeya, anatakiwa kurudi mjini na kuendelea kujifua, huu si muda tena wa kushangaa," alisema nyota huyo wa zamani wa Simba na Azam FC.

Ngasa alirejea Yanga akitokea Simba na katika mechi chache alizocheza, alisaidia timu yake kupata ushindi.

# Michezo

Jumamosi Aprili 18, 2020

Nipashe




Benzema ashikilia usajili wa Haaland UKURASA 22



Washambuliaji wa Juventus, Cristiano Ronaldo (kushoto) na Paul Dybala, wakishangilia bao katika mechi mojawapo ya Serie A msimu huu. **PICHA: MTANDAO**

# Simba yaiota UD Songo CAF

## ●●● Ni baada ya kuondolewa mapema na klabu hiyo ya Msumbiji katika Ligi ya Mabingwa Afrika...

**Na Somoe Ng'itu**

LICHA ya kuwa vinara na mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, uongozi wa Simba, umesema matokeo mabaya yanayowauma zaidi ambayo timu yao iliyapata msimu huu ni ya mechi ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya UD Songo ya Msumbiji, imefahamika.

**Simba ilitolewa mapema katika michuano hiyo baada ya kukubali sare ya bao 1-1 katika mechi ya nyumbani, wakati kwenye mchezo wa kwanza ugenini walitoka suluhu.**

Bao la kusawazisha la Simba lilifungwa kwa penalti na beki mkongwe, Erasto Nyoni katika kipindi cha pili.

Ilikuwa ni baada ya msimu uliopita chini ya Mbelgiji Patrick Aussems kufika hatua ya robo fainali ya michuano hiyo inayoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (Caf).

Akizungumza na Nipashe jijini Dar es Salaam jana, Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Haji 'De le Boss' Manara, alisema matokeo hayo yalikuwa ni 'katili' lakini yamewapa fundisho kuelekea msimu ujao wa michuano hiyo.

Manara alisema ili hali hiyo isijirudie, wachezaji wao watapambana kuhakikisha wanafanya vizuri zaidi katika msimu ujao ambao anaamini Simba itashiriki michuano hiyo.

"Mechi ambayo siwezi kuisahau msimu huu ni dhidi ya UD Songo, siwezi kuisahau," alisema Manara kwa kifupi.

Kiongozi huyo aliongeza matokeo ya mechi hiyo yalisaidia 'kuwaamsha' wachezaji wao na hivyo walipambana kusaka pointi tatu kwenye kila mchezo wa Ligi Kuu Bara waliocheza.

"Ingawa baadhi ya mechi tulipoteza, lakini maumivu yake hayafikii mechi ile ya Ligi ya Mabingwa Afrika, hatukupaswa kuishia pale tulipoishia, sio nafasi yetu kama Simba, hata wenyewe walijuwa walipata bahati," Manara alisema.

Hadi jana, Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), lilikuwa halijatoa mwongozo wowote kuhusiana na hatima ya Ligi Kuu Bara, Ligi Daraja la Kwanza, Ligi Daraja la Pili na mashindano ya Kombe la FA, ambayo bingwa mtetezi wake ni Azam FC.

Ligi Kuu hutoa mwakilishi wa Tanzania Bara katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika huku mshindi wa Kombe la FA hupata tiketi ya kushiriki michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika.

# Kado azitaja Simba, Yanga

**Na Mwandishi Wetu**

GOLIKIPA chaguo la kwanza wa Mtibwa Sugar, Shabani Kado, amesema katika maisha yake hakuwahi kuwaza kuzitumikia timu za Simba au Yanga, kama ilivyo kwa wachezaji wengine wa hapa nchini na badala yake alifikiria kuwa mwanamuziki.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Kado alisema mawazo ya kucheza mpira hayakuwa kwenye mipango yake ya maisha na muda mwingi aliwekeza katika kufanya kazi ya muziki.

Kado (pichani) alisema baadaye 'upepo' uligeuka na kujikuta anaingia zaidi kwenye mchezo wa soka na anashukuru Mungu kwa kupata nafasi ya kuitumikia Timu ya Taifa (Taifa Stars), wakati ikiwa chini ya Kocha Mkuu Mholanzi Mart Nooij.

Alisema alipokuwa Yanga, alikumbana na ushindani kutoka kwa golikipa Mghana Yaw Berko, lakini baadhi ya mechi alikuwa akilazimishwa kucheza baada ya kukataa kutokana na kuepuka lawama za wanachana na mashabiki wa klabu hiyo.



Aliweka wazi kipa huyo alikuwa "akisusa" kucheza mechi mbalimbali, hali iliyosababisha viongozi kumpatia fedha, jambo ambalo lilikuwa linawakera wachezaji wengine wa timu hiyo.

"Sikuwa na mawazo nayo, niseme ukweli, katika maisha yangu ningeweza kuwa mwanamuziki, katika Simba na Yanga hazikuwa kichwani mwangu, japokuwa mpira nimecheza, huyo Ali (Kiba), mimi alikuwa ananipitia tunaenda kucheza mpira," alisema Kado.

Aliongeza beki wake bora katika muda wote aliocheza ni Salum Swedi 'Kusi', ambaye aliwahi kucheza naye kwa mara ya kwanza akiidakia Stars dhidi ya Uganda, mechi iliyochezwa jijini Mwanza.

Kuhusiana na suala na ushirikiana kwenye mpira, Kado alisema binafsi yeye haamini kuwapo kwa jambo hilo lakini wapo wachezaji wenzake ambao wanafuatilia vitendo hivyo.

"Mpira wa kiafrika au Kitanzania, kuna majeraha ambayo ukipata, watu wanakwambia hiyo ni 'misumari', mimi katika maisha yangu nimewahi kupata majeraha mara mbili na mojawapo nikiwa Coastal Union,... sisi wenyewe wachezaji na watu wanaotuzunguka, ndio wanatuambiaga hivyo, ila mimi siamini," alisema Kado.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >